**MPANGO** atangaza kiama watendaji wa bodi za maji



UKURASA 3

**WAZIRI** Makamba: Safari za Samia zimeleta bil. 6/-

UKURASA 3

**BARAZA** la Uuguzi lafunguka chanzo wanafunzi wake kufeli kwa 66%

UKURASA 15



**FERNANDES AKIRI KUSHUKA KIWANGO**

UKURASA 22

Alhamisi Machi 21, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581622

# Nipashe

www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



UKURASA 2

# Kikokotoo bado moto

"Hili suala la kikokotoo linaweza kufanya watumishi walio kazini wakakosa uadilifu, pale wanapoona michango yao mwisho wa siku haikidhi matarajio ya kustaafu kwao."

**Doroth Semu, Kiongozi wa ACT Wazalendo**

## DC ALIYENUSURIKA AJALI ASHANGAA HAKUIBIWA

UKURASA 7



Wananchi wakiangalia gari la Mkuu wa Wilaya ya Musoma, mkoani Mara, Dk. Khalfan Haule (hayupo pichani), baada ya kupinduka katika Kijiji cha Kwikuba juzi, wakati akitoka Musoma Vijijini kukagua miradi ya maendeleo. Kwa mujibu wa mkuu huyo, chanzo cha ajali ni kupasuka kwa tairi la kushoto mbele, ambapo yeye na dereva wake walipata majeraha kutokana na kukatwa na vioo. Habari Uk. 7. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA 2

# Nusu ya wanaochunguzwa wabainika meno yameoza

## Mafuriko Kilosa, 1,400 wakosa makazi na vyoo

UKURASA 5

**MICHEZO** SIMBA: TUNAITAKA NUSU FAINALI AFRIKA UK. 24

**KATUNI** UK. 6

HABARI KITAIFA



Bingwa wa Kinywa na Meno kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH-Upanga), Dk. Germana Lyimo (kushoto), akichunguza kinywa cha mmoja wa wakazi wa Mkoa wa Pwani, waliofika eneo la Maili Moja, wilayani Kibaha jana, kwenye kambi ya uchunguzi katika kilele cha maadhimisho kitaifa ya Siku ya Afya ya Kinywa na Meno Duniani, iliyoandaliwa na Chama cha Wataalamu wa Afya ya Kinywa na Meno Tanzania (TDA) pamoja na Wizara ya Afya. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Kikokotoo mafao bado ngoma ngumu

**Na Joyce Lameck**

KIKOKOTOO cha mafao ya wastaafu bado kinaumiza vichwa wadau, safari hii Chama cha ACT-Wazalendo kikitaka serikali kufanya tena marekebisho ya sheria ili kurejea katika kikokotoo cha awali.

Chama hicho kina hoja kwamba, kama kikokotoo cha sasa cha asilimia 33 kitaendelea kutumika, kuna hatari watumishi wakakosa uadilifu wakitambua kwamba watakapostaafu, watakachopewa kutokana na michango yao hakitakuwa na tija.

Hilo ni sehemu ya aliyoelekeza Kiongozi mpya wa ACT-Wazalendo, Doroth Semu, alitangaza mawaziri kivuli wapya aliowateua jana jijini Dar es Salaam, akiwataka wakazisemee changamoto za wananchi.

Akiainisha maeneo mahsusi ya kutupia jicho wakati wote wa utumishi wao katika nafasi hizo, Doroth aliwaelekeza kuwa maeneo muhimu wanayopaswa kuyasimamia ni pamoja na kutaka sheria ya kikokotoo ibadilishwe na kurejeshwa sheria ya zamani kwa ajili ya kulinda maslahi ya wafanyakazi.

Alisema kikokotoo kipya kinaathiri watumishi walio kazini na waliostaafu na kueleza kuwa kanuni hiyo inaweza kufanya watumishi wasiwe waadilifu katika utendaji kazi wao.

"Nendeni mkawe sauti ya wananchi, hili suala la kanuni mpya ya kikokotoo ni lazima serikali iliangalie upya, linaweza kufanya watumishi walio kazini wakakosa uadilifu, pale wanapoona michango yao mwisho wa siku haikidhi matarajio ya kustaafu kwao," aliagiza Doroth.

Tangu mwaka 2018, kikokotoo kipya cha mafao ya wastaafu kimekuwa kinaibua mvutano wa serikali na wadau wa masuala ya hifadhi ya jamii.

Ni mvutano uliosababisha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli kuingilia kati na kuagiza matumizi kikokotoo cha asilimia 25 (kutoka asilimia 50 ya awali) yasogezwe hadi mwaka 2023 na ilipotimu mwaka huo, serikali ilitangaza kikokotoo kipya cha asilimia 33 ambacho bado kinapingwa na baadhi ya wadau, ikiwamo ACT Wazalendo.

Mbali na kikokotoo, Doroth pia alielekeza mawaziri kivuli aliowateua, kipaumbele mwaka huu kiwe kuendelea kupigania unafuu wa gharama za maisha, kushinikiza serikali kutazama upya bei ya nauli za mabasi na daladala nchini na kutokupatikana uhakika wa umeme.

Vilevile, Doroth aliwataka mawaziri kivuli kupigania haki za usalama mijini na vijijini ili kumaliza migogoro ardhi, kupinga ubadhirifu serikalini na kushinikiza serikali kutengeneza ajira ili kutatua tatizo la uhaba wa ajira, hususani kwa vijana.

Akifafanua kuhusu ajira, Doroth aliwataka mawaziri kivuli walioteuliwa wawe chachu ya kuishinikiza serikali kuhakikisha mifumo ya ajira inaimarishwa huku akieleza kuwa mfumo wa sasa unaliacha kundi kubwa la wasomi wa ngazi tofauti likiwa mitaani.

"Tunaona majina hata ya wanaoteuliwa ni yaleyale, wapo wanaoboronga sehemu moja na kwenda sehemu nyingine, majina yanazunguka tu huku vijana wakiachwa, wanaopewa nafasi katika mifumo ya serikali ni walewale, hata kama wanaharibu, hakuna anayeachwa pembeni," alisema.

Kuhusu ufisadi, Doroth alisema "ni jambo la kusikitisha kuona kelele za ufisadi zinazoanzia Ofisi ya Rais - TAMISEMI hazichukuliwi hatua ipasavyo licha ya tume kadhaa kuonesha uhusika wa baadhi ya watumishi wa wizara hiyo wakishirikiana na maofisa wa halmashauri kujichotea fedha.

"TAMISEMI ipo chini ya Rais, watumishi wanaochezea mifumo ya Tehama kwa kushirikiana na maofisa wa halmashauri wapo chini ya ofisi hiyo na hakuna aliyewajibishwa mpaka wakati huu," alisema.

Baraza kivuli la mawaziri la ACT Wazalendo lilianzishwa mwaka 2022 baada ya matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa 2020 kukosa uwakilishi mkubwa wa upinzani bungeni.

Lililotangazwa jana ni la pili tangu azimio la Halmashauri Kuu ya chama. Doroth alilitaja kuwa kwa miaka miwili limekuwa na mchango mkubwa kwa chama na taifa.

Alisema kuwa katika miaka miwili ya utendaji wa baraza hilo, waliweka nguvu kuwasemea wananchi kwenye migogoro ya ardhi, malalamiko na madai ya wafanyakazi nchini, kupanda kwa gharama za maisha, bima nafuu na uhakika wa bei za mazao kwa wakulima.

"Kuna baadhi ya hoja zilifanikiwa kuchukuliwa na serikali kuzifanyia kazi; ruzuku kwenye mbolea pamoja petroli na dizeli, kuondolewa kodi kwenye mafuta ya kula na kulikoshusha bei yake, kupunguzwa tozo za miamala ya simu, serikali kuiwezesha NFRA (Wakala wa Taifa wa Hifadhi Chakula) kununua vyakula ili kushusha gharama nchini," alisema.

Doroth alisema baraza hilo pia limekuwa sauti kuu ya chama hicho katika kukosoa sera za chama kilicho madarakani, likipendekeza na kushawishi sera mbadala tangu kuundwa kwake.

Katika nafasi hizo alizoteua jana, wamezingatia usawa wa kijinsia na kuwapa wanawake kipaumbele kwa asilimia 52, pia wameendelea kuwaamini vijana kwa kuwapa nafasi katika baraza hilo kwa asilimia 47.

Baraza jipya la Mawaziri Kivuli lililotangazwa jana na Doroth, linajumuisha Waziri Mkuu Kivuli, Isihaka Mchinjita na Katibu Mkuu Kiongozi, Idrisa Kweweta. Lina jumla ya wizara 24.

## Nusu ya waliochunguzwa wabainika meno yameoza

**Na Christina Mwakangale,** KIBAHA

WATU 1,666 waliofanyiwa uchunguzi wa magonjwa ya kinywa na meno, wamebainika wana tatizo la kuoza meno.

Idadi hiyo ni kati ya 3,297 waliojitokeza kuchunguzwa na miongoni mwao 358 wana tatizo la magonjwa ya fizi huku 119 walibainika kuwa na tatizo la mpangilio mbaya wa meno.

Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Kinywa na Meno, Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, alibainisha takwimu hizo jana, kwenye maadhimisho kitaifa ya Siku ya Afya ya Kinywa na Meno Duniani, wilayani hapa, mkoani Pwani.

Alisema watu 8,528 wamefikiwa na huduma hiyo katika kambi hiyo, iliyoandaliwa na Chama cha Wataalamu wa Afya ya Kinywa na Meno Tanzania (TDA) pamoja na Wizara ya Afya.

"Watu 133 sawa na asilimia 4.0 wamekutwa na tatizo la mapengo katika kambi ya elimu ya afya ya kinywa na meno kwenye vituo vitano vya watu wenye mahitaji maalum na shule za msingi, tumewafikia watu 8,528 kuanzia Machi 14 hadi 20, mwaka huu, kwa kuwapatia matibabu bure.

Pia katika kipindi hicho cha wiki moja, watu 249 waliochunguzwa, walioóza meno walitibiwa kwa kuzibwa.

Alibainisha kuwa watu 598 sawa na asilimia 35.9 ya waliofanyiwa uchunguzi meno yao kubainika yameoza waling'olewa, 133 walitengenezewa meno bandia baada ya kukutwa na mapengo.

"Watu 84 sawa na asilimia 23.5 ya wenye magonjwa ya fizi walisafishwa meno na 29 ambao ni asilimia 1.7 ya walioóza meno walipatiwa matibabu ya mzizi wa jino.

Awali, mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Nickson Simon, alitoa wito kwa jamii kujenga tabia ya kufanya uchunguzi wa afya ya kinywa na meno na kupata matibabu.

Rais TDA, Dk. Gema Belege, alisema takribani wataalamu 80 wa kinywa na meno, walitoa huduma ya afya ya kinywa na meno kwa wananchi wa mkoani hapa, katika vituo vya huduma, ikiwamo Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani Tumbi, Hospitali ya Wilaya ya Lulanzi na kituo cha afya cha Mkoani.

"Tulitembelea shule za msingi tisa, vituo vya kulelea watoto wenye mahitaji maalumu saba, ambako tumetoa elimu na kufanya uchunguzi wa afya ya kinywa na meno na waliobainika walipatiwa huduma," alisema Dk. Gema.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba (kulia), akifanya mahojiano maalum na Mhariri wa Habari wa gazeti hili, Salome Kitomari, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: CARLOS BANDA**

# Makamba: Safari za Samia zimeleta bil. 6/-

**Na Salome Kitomari**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, amesema ziara za Rais Samia Suluhu Hassan zimeiwezesha nchi kupata miradi ya zaidi ya Sh. bilioni sita na mtaji unaoingizwa nchini kukua kutoka Sh. bilioni moja mwaka 2020 hadi bilioni 6.5 mwaka huu.

Akizungumza jana katika mahojiano maalum na waandishi wa habari wa kampuni ya The Guardian Limited kuhusu miaka mitatu ya Rais Samia madarakani, Makamba alisema miradi mingi ni yenye kubadilisha maisha ya Watanzania na kukuza uchumi wa nchi.

"Hizi ziara zina manufaa makubwa na ya moja kwa moja, mfano hivi karibuni alienda Morocco kwenye mkutano wa African Investment Forum, ambako alikuwa na mazungumzo ya miradi mingi duniani. Lakini alikuwa na miradi yake ambayo ni Bandari ya Mangapwani Zanzibar, reli mpya kutoka Ziwa Nyasa Mbaba Bay hadi Songea, Mchunguma hadi Mtwara.

"Alikuja na mradi wa kipande cha SGR Kigoma hadi Burundi na kwamba ilipokelewa na kupata fedha kwa mikopo nafuu. Nina mifano mingi sana ya Rais Samia anavyokuwapo kwenye mikutano anawezesha upatikanaji wa fedha za miradi mingi kwa ajili ya nchi. Kwa safari hii moja tulipata miradi ya Sh. bilioni sita," alisema.

Kwa mujibu wa Makamba, kila wanapofanya ziara nje ya nchi wanakutana na wawekezaji, wanafanya kongamano la biashara la uwekezaji na lengo ni kuhakikisha nchi inanufaika.

"Mfano mwaka 2020 kiwango cha mtaji ulioingia hapa nchini ulikuwa Dola bilioni moja, lakini mwaka jana tumeingiza Dola bilioni 5.6, kutokana na ushawishi wa yeye kwenda, wawekezaji kubwa duniani wanachohitaji ni kumuona Rais, kumsikia, kumtazama usoni na kumsikia kauli yake basi," alisema.

Waziri Makamba ambaye ni Mbunge wa Bumbuli alisema viongozi wengi wanaweza kwenda na kuzungumza, lakini watu wanaamini sana mkiwa na Rais, ndio maana kiwanda cha mtaji kilichoingia kimeongezeka.

"Safari hizi hii ina maana gani? Mapato ya serikali yameongezeka ambayo yatawezesha kujenga zahanati, kuchonga barabara, elimu bure, kufikisha umeme vijijij, kutengeneza madawati na kununua dawa zaidi. Mfano biashara kati ya India na Tanzania ilikuwa inasuasua, tumeenda kule Rais ametoa ushawishi na sasa mbaazi nyingi inanunuliwa.

"India inalima mbaazi pia, hivyo inatoa nafasi ndogo kwa baadhi ya nchi na kwamba kuwa ziara ya Rais Samia sasa tunauza mbaazi nyingi na wananchi maisha yao yamebadilika na kununua vyombo vya usafiri, kujenga nyumba zao na kuhudumia familia zao. Utaona kuna faida ya moja kwa moja kutokana na ushawishi.

"Watu wengi hawajui kwamba hakuna hata nafasi ya kupumua tunaposafiri, anatoa mkutano huu na kwenda mwingine, akifika kwenye ndege amechoka (Rais Samia) kabisa. Sisi tunaona manufaa makubwa sana na wakati mwingine tunatamani twende naye kila mahali kwa sababu kazi inakuwa rahisi zaidi," alisema.

**SARAFU YA EAC**

Waziri Makamba alisema sarafu ya pamoja ni sehemu ya mchakato wa kufikia kilele cha utangamano wa Afrika Mashariki, na kwamba sarafu ya pamoja ni hatua mojawapo na kwamba kuna vigezo vinavyotakiwa.

"Ili muwe na sarafu moja lazima uchumi wa nchi zote uwe umefikia uwezo fulani na kwamba kwa sasa thamani ziko tofauti, ile ni safari ya pamoja ni kweli ilitakiwa iwe 2024 na sasa imesogezwa 2031, maana yake hatukufikia vigezo, sio kwamba hatukutaka ila hatukufikia vigezo vya pamoja.

"Mwaka 2031 ni kutoa nafasi nchi zote zifikie kwa pamoja, Tanzania wajibu wetu ni kufikia vigezo vya kiuchumi ikiwamo sera za fedha na mfumuko wa bei. Lakini kuna vigezo wa kitaasisi kama kuunda taasisi moja ya fedha kama kuwa na Benki Kuu moja ili kudhibiti sarafu," alisema.

Hivi karibuni, zilisambaa noti mbalimbali mtandaoni zikitajwa kuwa ndio fedha ya EAC lakini kiongozi huyo alikanusha.

**MAENEO YA KUJIVUNIA**

Waziri Makamba alisema kuimarisha mahusiano kati ya Tanzania na nchi nyingine, taasisi za kimataifa na mashirika makubwa duniani, na ushahidi wa kuimarika kwa uhusiano huo ni ziara zilizofanywa na marais mbalimbali waliokuja nchini na ambazo Rais Samia amezifanya nchi ikilinganishwa na miaka mitatu iliyopita.

"Lingine ni biashara na uwekezaji vimeongezeka na kupanuka kutokana na kazi anayoifanya Rais ya diplomasia ya uchumi ambayo moja ya malengo ni kuongeza biashara na kuongeza mtaji unaoingia ambao ili uje unahitaji ushawishi mazingira ya biashara, nchi inatawaliwa kwa utawala wa sheria na kupata faida," alisema.

Alisema lingine ni sauti na kauli ya ushawishi wa nchi kwenye masuala mtambuka kama nishati safi ya kupikia, mabadiliko ya tabianchi, usawa wa jinsi, usalama wa chakula, raslimali watu ambayo Rais amesema na kushiriki.

"Moja ya vielelezo vya mafanikio kwenye diplomasia ya nchi ni nchi yenu au kiongozi wenu kutakiwa uongozi wake au kauli yake au msaada wake kwenye masuala mtambuka ya duani nchi zinashirikiana, Nchi yetu sauti yake imesikika," alibainisha.

Alisema lingine ni kuongezeka na kupata raslimali za kugharamia shughuli za maendeleo na kwamba kupitia ushawishi wa kidiplomasia na uhusiano bora na ndio mana miradi ya kimkakati imepata fedha na kwmaba mifuko mbalimbali na taasisi duniani zinatoa fedha.

La tano ni kuimarisha ujirani mwema na amani na usalama na kwamba msingi mkubwa ni ujirani mwema na majirani kwa kuwa na maelewano na kuleta amani kwenye ukanda huo.

# Watendaji bodi za maji watangaziwa kiama

**Na Mary Mosha, HAI**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameagiza kufukuzwa kazi kwa watendaji wa bodi za maji watakaobainika kuwabambikizia wananchi bili, kuwatoza gharama kubwa wakati wa kufungiwa huduma na wanaochukua muda mrefu kutekeleza kazi hiyo.

Bodi hizo za maji zinasimamia miradi ya maji chini ya Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA).

Dk. Mpango aliagiza hayo jana wakati akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji cha Kwa Sadala baada ya kuzindua mradi wa maji wa Sh. bilioni 3.3 utakaowanufaisha zaidi ya wananchi 63,000 wa kata tatu za wilaya ya Hai.

"Waziri wa Maji (Jumaa Aweso), usiwafumbie macho watu hao. Tuma hata makachero wako wafuatilie kuona kama bili za maji ni halisi na gharama za uvutaji wa maji. Ila niongeze aliyeomba kuvuta maji zisizidi siku saba. Weka nguvu kubwa hapa ile dhana ya kumtua mama ndoo kichwani ionekane kwa vitendo. Asivumiliwe mtu.

"Mkoa wa Kilimanjaro, hasa Wilaya ya Hai, kama huu moto unaolipuka lipuka kwenye Mlima Kilimanjaro, ukiendelea hatufiki. Tutapoteza utalii lakini kubwa zaidi haya maji tumezindua leo yatapotea.

Kwa hiyo tunaowajibu wakupanda miti, kutunza miti na misitu yetu iliyopo pembezoni mwa mlima na vyanzo vya maji, ili tuendelee kupata maji," alisema,

Waziri Aweso alisema mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 na umegharimu Sh. bilioni 2.8, ingawa ulitengewa bilioni 3.3. fedha zilizobaki katika mradi huo ni Sh. milioni 500.

"Tunatambua mradi huu wa maji utasimamiwa na Bodi ya Uroki (Bomang'ombe/Uroki Water Trust), viongozi naomba mnisikilize kwa makini. Ni haki ya mwananchi kupata maji na ni wajibu wa mwananchi kulipia maji.

Lakini ni marufuku bodi kumbambikizia mwananchi bili za maji, wala kumwekea mwananchi gharama kubwa anapotaka kuunganisha maji majumbani. Sisi viongozi wa maji hatutakuwa vikwanzo kwa wananchi kupata huduma ya maji, lazima tuweke bei halisia na suala la kumuunganishia maji lisizidi siku saba," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema amemweleza Makamu wa Rais kuwa wakazi wa mkoa wanaomba serikali kusukuma mradi wa ujenzi wa barabara ya Arusha - Moshi - Holili kuanza rasmi baada ya kusimama kwa muda mrefu.

Akiunga mkono kauli hiyo, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi alisema: "Mheshimiwa Makamu wa Rais, tunaiomba serikali kufanya jambo, kabla ya kwenda kwenye uchaguzi mkuu.

"Tayari wapo wananchi ambao walifanyiwa tathimini kupisha mradi huo na wengine hawalimi. Hawafanyi maendeleo na fidia bado haijatoka na limechukuwa muda mrefu."

# TALGWU yalaani mfanyakazi mwenzao kuuawa na wafugaji

**Na Christina Haule,** MOROGORO

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU), kimelaani mauaji ya mwanachama na kiongozi wao, Madadi Litumbui kwa kuchomwa mkuki na mfugaji wakati wakiwaondoa wafugaji katika msitu wa serikali uliounganisha vijiji na kuwa hifadhi moja wilayani Kilwa, mkoani Lindi.

Akitoa tamko hilo mbele ya waandishi wa habari, Katibu Mkuu wa TALGWU, Rashid Mtima alisema, tukio hilo lilitokea Machi 17, mwaka huu, wakati mtumishi huyo akiwa doria na wenzake alichomwa mkuki na kukimbizwa Kituo cha Afya Nanjilinji (Kilwa) na kufariki dunia usiku huo.

"Tumepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha mwanachama na kiongozi wetu ndugu Medadi aliyekuwa Mtendaji wa Kijiji cha Mtumbei, huku akihudumu TALGWU kwa nafasi ya Katibu wa Kamati ya Uratibu Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa," alisema.

Mtima alisema Litumbui alifariki dunia wakati akitekeleza majukumu yake kama Mtendaji wa Kijiji cha Mtumbei Mpopela, Kata ya Kandawale Tarafa ya Kipatimu, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Aliiomba polisi kuongeza nguvu ya kumtafuta mfugaji huyo wa jamii ya kimang'ati aliyemrushia mkuki mtumishi huyo na kumsababishia umauti.

"TALGWU inalaani vikali mauaji ya mwanachama wetu ndugu Madadi na itafuatilia kwa ukaribu kuhakikisha haki inatendeka, aidha tunaliomba Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wale wote walioshusika na mauaji hayo ya kinyama," alisema Mtima.




Ofisa wa masuala ya sheria wa GGML, Elizabeth Karua (katikati), akishiriki mdahalo kuhusu ushiriki wa wanawake katika sekta ya madini ulioandaliwa na Taasisi ya Women in Management Africa (WIMA), jijini Dar es Salaam, katika mwendelezo wa kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani. Kulia ni Mkurugenzi wa Ushauri wa Mnyororo wa Ugavi wa Kampuni ya ASNL, Humphrey Simba na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Business Women of Africa Collective Capital, Gugu Ntuli. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Elimu ni mkombozi kwa wanawake'

**Na Mary Geofrey**

MTOTO wa kike akisomeshwa anaongeza uwezo wa kujiamini na kushika nafasi za juu za uongozi kwa maendeleo ya familia na jamii.

Imebainishwa kuwa kwa sasa ni asilimia 32 tu ya wasichana wanaohitimu elimu ya kidato cha nne, hivyo kuhitajika msukumo kwa wazazi na walezi kusomesha watoto wao.

Hayo yalibainishwa juzi wakati wa mdahalo uliohusisha Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) pamoja na Taasisi ya Women in Management Africa (WIMA), ukiandaliwa na taasisi hiyo ikiwa ni mwendelezo wa kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani.

Mdahalo huo uliodhaminiwa na GGML, ulikuwa na mada mbalimbali ikiwamo ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi, biashara na masuala ya uhifadhi wa mazingira.

Akichangia mdahalo huo, Ofisa wa Masuala ya Sheria wa GGML, Elizabeth Karua, alisema ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika sekta ya madini, kampuni hiyo hutoa kipaumbele kwa wanawake katika nafasi za kazi ambapo mbali na kuwapa wanawake asilimia 50 ya nafasi hizo, pia wanapofungana na wanaume katika usaili, wanawake hupewa kipaumbele.

"Mazingira ya kazi ndani ya GGML yameendelea kuwa rafiki kwa wanawake hasa ikizingatiwa hata nafasi ya usimamizi wa idara mbalimbali ndani ya kampuni zinashikwa na baadhi ya wanawake huku wengine wakifanikiwa kuvuka mipaka na kwenda kuwa mameneja kwenye kampuni nyingine," alisema.

Makamu Rais wa AngloGold Ashanti - GGML anayeshughulikia miradi endelevu na masuala ya ubia na ushirika Afrika, Simon Shayo, alisema "ndani ya Kampuni ya AngloGold Ashanti kumekuwa na sera na miongozo ambayo si tu imeongeza idadi ya ushiriki wa wanawake kwenye shughuli za madini, bali pia imeweza kubadili tabia za wanaume waliopo kwenye mgodi wetu na kuona umuhimu wa ushiriki wa wanawake katika shughuli za uchimbaji."

Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa GGML, Stephen Mhando, alisema mgodi huo ndio unaoongoza nchini kwa kutoa fursa kwa wanawake nchini.

Alisema asilimia 13 ya wafanyakazi wa mgodi huo ni wanawake na wamepewa nafasi za juu za uongozi, jambo ambalo linazidi kutoa motisha hata kwa wanawake wengine kujiunga na sekta hiyo ya madini.

"GGML ambayo imeendelea kuwa mdhamini kwa matukio ya Taasisi ya WIMA, tunajivunia kuonesha kuwa namna gani tunawajali kinamama na kufanya nao kazi kwa ukaribu. Ukilinganisha tulipotoka na tulipo ni hatua kubwa kwani wanawake wapo wachache, lakini wapo kwenye sehemu ambazo wanaongoza watu," alisema.

Mwongoza mdahalo huo ambaye ni Mkuu wa Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere, Prof. Marcellina Chijoriga, aliwasihi wazazi kuwekeza katika kusomesha mtoto wa kike kwa kuwa elimu ndiyo itakayomwezesha kushiriki nafasi mbalimbali za juu za uongozi.

"Wito wangu kwa mama na baba, somesha mtoto wako wa kike awe bora... ili afike mbali, ukiwekeza kwa mtoto wa kike umewekeza kwenye familia na mama kwa ujumla," alisema.

Alitoa wito kwa wanawake kujifunza kushirikiana na kuingia kwenye masuala ya kiuongozi.

"Kujiamini kwangu ndio kumenifanya niweze kufanya kazi na marais wanne. Uwezo wako unatokana na wewe. Hivyo, ninamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kuniteua kuwa Mkuu wa Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo ya WIMA, Naike Moshi, alisema changamoto kubwa kwa wanawake ni ukosefu wa elimu.

Alisema hadi sasa ni asilimia 32 tu ya wasichana wanaohitimu elimu ya kidato cha nne, hivyo ni wazi bado msukumo mkubwa unahitajika kwa wazazi na walezi kusomesha watoto wao.

# Kampuni ya Kitanzania yashinda zabuni kusafirisha mizigo reli ya TAZARA

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya Kitanzania imeshinda zabuni ya kusafirisha mizigo kutoka Tanzania kupitia Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Zambia na nyingine za SADC.

Kampuni hiyo ya Bravo Group, inaongozwa na Mwenyekiti, Angelina Ngalula ambaye pia ni Mwenyekiti mstaafu wa TPSF.

"Sisi tuko tayari kuleta treni nyingi zaidi katika njia hii, lakini kutokana na changamoto ya njia tutaanza na treni mbili ambazo zitakuwa zinapishana," alisema Angela.

Alisema treni moja itakuwa inabeba mabehewa 20, na kila behewa litakuwa na uwezo wa kupakia tani 50.

"Kwa hiyo treni moja itakuwa inabeba tani 1000, sawa na malori 40 na kwa jinsi TAZARA watakavyoendelea kuboresha njia za reli ndivyo na sisi tutakavyokuwa tunaongeza treni," alisema Angela.

Alisema wako tayari kuanza kazi hiyo wakati wowote.

"Tulichokuwa tunasubiri sisi ni tukio la leo la kusaini mikataba na kwa sababu hili limefanyika, tunasubiri wenyewe TAZARA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), baada ya kumaliza taratibu zao za ndani waturuhusu tuendelee," alisema.

"Lakini sisi tuko tayari wakati wowote hata wakituambia tuanze kesho kwa sababu treni zipo tayari na tulilisubiria hili kwa muda mrefu."

Alisema mpango wao ni kutoa mizigo moja kwa moja kutoka Bandari ya Dar es Salaam kuipeleka nje katika nchi hizo za SADC.

Alisema mizigo mikubwa watakayokuwa wanasafirisha ni madini pamoja na mazao ya kilimo.

"Sisi tuna 'deal' sana na kampuni kubwa za nje ya nchi hususani Congo na Zambia, zinazofanya biashara ya madini. Kwa hiyo tutakuwa tunabeba mizigo ya madini na mazao ya kilimo," alisema.

"Na tumepata nguvu yote hii kwa sababu serikali imeweka mazingira mazuri kwa sasa ya kufanyia biashara. Rais Samia Suluhu Hassan ametuamini sisi sekta binafsi na kutuwekea mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji na sisi hatutamwangusha," alisema Angela.

Mkurugenzi wa TAZARA, Bruno Chingandu, alisema zabuni hiyo ilikuwa ya ushindani na ilifanyika kwa uwazi na ilishindanisha kampuni nyingi kutoka ndani na nje ya Tanzania.

"Kwa kweli ni fahari na inatia moyo sana kuona Mtanzania ameshinda zabuni kubwa namna hii, tena ambayo ilishindanisha kampuni kubwa za ndani na nje ya nchi, hili ni jambo la kihistoria na ni vema Watanzania wengine wajifunze," alisema.

Mjumbe wa Bodi TPSF, Octavian Mshilu, alisema TAZARA ni mwendeshaji wa kwanza katika sekta ya reli nchini kushirikisha sekta binafsi hasa katika zabuni kubwa namna hiyo.

Mshilu alisema hiyo ni hatua kubwa na itachangia kwa kiwango kikubwa kuwatia moyo na kuwavutia wawekezaji wengine katika sekta hiyo na nyinginezo.

HABARI KITAIFA

# Mbarawa: Changamkieni fursa za uwekezaji SGR

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa amewataka wawekezaji kuchangamkia fursa katika sekta ya uchukuzi, utalii na usafirishaji zitakapoanza safari za treni ya kisasa ya umeme.

Alitoa rai hiyo juzi mkoani Morogoro baada ya kukamilika awamu ya pili ya majaribio ya treni ya umeme kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro iliyotumia saa mbili kutoka Dar es Salaam, akiambatana na madiwani 10 wakiongozwa na Meya wa Jiji hilo, Omary Kumbilamoto.

Prof. Mbarawa alisema Morogoro ni miongoni mwa mikoa ambayo ina fursa nyingi za kiuchumi, lakini hazijazitumika, hivyo ujio wa treni hiyo utachochea wawekezaji zaidi na kufungua fursa mbalimbali zikiwamo za utalii na kilimo pamoja na mazao yake.

"Morogoro ni moja ya maeneo ya kimkakati ya kiuchumi ambayo ukusanyaji mizigo na huduma mbalimbali upo kwa kiwango kikubwa. Ninatoa wito kwa wakazi wa maeneo haya kushiriki kikamilifu katika uzalishaji ili kuhakikisha SGR inapata mizigo ya kutosha pale inapoanza," alisema Prof. Mbarawa.

Alisema tayari Shirika la Reli Tanzania (TRC) limejenga kituo cha kukusanya mizigo itakayosafirishwa kutoka mkoani humo hadi Dar es Salaam au sehemu nyingine ya nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alisema mipango inaendelea kuhakikisha Kilosa na Mikumi zinaunganishwa na SGR ili kutumia fursa za kiuchumi ambazo hazijatumika.

"Mamlaka ya mkoa iko katika mazungumzo na waendeshaji watalii ili kukifanya kituo cha Kilosa kuwa kituo cha utalii kwa wale wote wanaotarajia kutembelea vivutio vya utalii vya mikoani.

"SGR itakuwa uti wa mgongo wa uchumi wa eneo letu katika siku za usoni. Tuna mashamba ya miwa na uzalishaji mkubwa wa mpunga. Haya yote yatasafirishwa kwa njia ya reli ili kupunguza msongamano barabarani na pia gharama ya usafirishaji," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, alisema katika majaribio ya treni hiyo awamu ya pili, ilivuta mabehewa 14 baada ya manne katika awamu ya kwanza.

Kadogosa alisema kuwa katika majaribio ya awamu ya pili, treni hiyo ilisafiri kwa kasi ya 120 na 160 kwa kilometa kwa saa na kuongeza kuwa mara majaribio yatakapokamilika, itasafiri kwa kasi ya 160 kwa saa.

"Tunajaribu mabehewa yetu 14 ya abiria baada ya injini za treni kufanya majaribio kwenye mfumo wa umeme. Nia yetu kwamba ifikapo Julai mwaka huu, shughuli hiyo itaanza," alisema.

Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto, alisema uendeshaji treni hiyo mpya ya umeme utachochea fursa nyingine za kiuchumi, ikiwamo kibiashara na usafiri.

# Mafuriko Kilosa, 1,400 wakosa makazi na vyoo

**Na Beatrice Shayo**

JUMLA ya watu 1,404 wameathirika na mafuriko ya mvua inayoendelea kunyesha Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro huku nyumba 351 zikiingia maji na vyoo 368 kubomoka.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Shaka Hamdu Shaka, akizungumza na Nipashe alisema, kaya zilizoathirika ni 368 na nyumba 17 zimebomoka.

Alisema kitongoji cha Kampala, kaya 161 na watu 624 wameathirika, kitongoji cha Madizi kaya 137 zimeathirika na watu 531, kitongoji cha Estate kaya zilizoathirika 57 na watu 196 wamepata madhara.

Alitaja kingine kilichopata maafa hayo kuwa ni cha Lugunga baada ya kata nane na watu 32 kuathirika, kitongoji cha PWD, kaya tano na watu 20 wameathirika.

Shaka alisema nyumba 17 zilizobomoka, tano zinatoka kitongoji cha Kampala, nyumba nane kitongoji cha Estate na nyumba nne kitongoji cha Madizini.

Alisema jumla ya vyoo 368 vimebomoka kutokana na mafuriko na kusababisha maji kuchafuka.

Aidha, Shaka alisema jumla ya visima 30 vya maji vinavyotumika vimeathirika na mafuriko hayo kwa kuingiliwa na maji machafu.

Akizungumzia hali ya miundombinu ya barabara, Shaka alisema barabara ya mita 1,700 za barabara ya Mikumi - Kilosa, zimeathirika kwa maji yaliyokata barabara na kusababisha kukatika mawasiliano baina ya Kilosa na Mikumi hali iliyosababisha usumbufu kwa abiria na mizigo yao.

Alisema Machi 17, mwaka huu maji mengi yalijaa katika mto wa Miyombo unaopita katika vijiji vya Ulaya, Zombo na Changarawe baada ya mvua kubwa kunyesha katika vijiji vya Kisanga, Madizini na Kitunduweta.

Alisema mvua hiyo ilisababisha athari katika makazi, mashamba na miundombinu ya maji na barabara katika kijiji cha Changarawe.

Shaka alisema kijiji cha Changarawe kimekuwa na matukio ya kupatwa na mafuriko mara kwa mara tangu mwaka 2016 na msimu huu wa mvua tangu Desemba, mwaka jana, hadi sasa ni tukio la tisa la mafuriko.

"Mafuriko haya yamesababishwa na maji kujaa katika mto Miyombo nje ya kingo za mto baada ya ongezeko la kujaa mchanga katika mabwawa ya Nara na Kipera ambayo yalichimbwa kwa ajili ya kupunguza kasi ya maji kipindi cha mvua kubwa na kuruhusu maji machache kuingia katika mto huo," alisema Shaka.

Shaka alisema uharibifu wa tuta hilo lililojengwa pia kuzuia maji yasiingie katika mashamba ya mkonge enzi hizo kwa sasa yamekuwa ni makazi ya watu.

Aidha, alisema shughuli za kibinadamu katika kingo za mto huo ambapo wakazi wa eneo hilo hulima na kuchunga katika tuta hilo wameathiriwa na mvua hizo.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo, Stella Kahwa, akishuhudia kazi ya uhakiki wa mita za umeme 500 zilizoanza kuhakikiwa na wataalamu wa taasisi hiyo, kupitia kituo chake cha upimaji cha Misugusugu, mkoani Pwani jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Jafo aagiza usimamizi wa miradi ya EBARR

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kusimamia Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (EBARR) kuhakikisha unatekelezwa kwa ubora na kwa wakati ili kufikia malengo ya serikali ya utunzaji wa mazingira.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, alitoa kauli hiyo juzi alipokagua na kuzindua miradi mbalimbali kupitia EBARR katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha miradi hiyo pamoja na kuwa endelevu, iwanufaishe wananchi katika maeneo inakotekelezwa.

Kutokana na hayo, Dk. Jafo alitaka wasimamizi wa miradi hiyo kwenye halmashauri za wilaya kuhakikisha wanaisimamia inavyotakiwa kwa kuwa inagusa eneo kubwa la maisha ya watu.

"Serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kulinda mazingira ukiwamo huu wa EBARR, hivyo sote hatuna budi kuitekeleza ipasavyo ili tija na thamani vipatikane kwa wananchi," aliagiza.

Diwani wa Ngh'ambi, Richard Matonya alisema mradi wa kisima kilichochimbwa katika eneo hilo umesaidia upatikanaji huduma ya maji kwa urahisi.

Alisema kuwa awali wananchi walikuwa wanakwenda kuchota maji umbali wa zaidi ya kilometa 10, lakini kwa sasa wanaweza kupata huduma hiyo karibu na maeneo yao.

Pia alisema mradi huo wa kisima umewezesha wananchi kujishughulisha na kilimo cha mboga na kuachana na shughuli za uharibifu wa mazingira hususan ukataji miti.

Mratibu wa EBARR Kitaifa, Dk. Makuru Nyarobi, alisema lengo la miradi hiyo ni kusaidia wananchi katika shughuli zao hasa katika kuwainua kiuchumi, ndio sababu wamejielekeza zaidi vijijini.

Alisema kuwa kupitia mradi huo, wananchi wamekabidhiwa vyerehani kwa ajili ya kujishughulisha na shughuli mbadala zikiwamo ushonaji na hivyo kuachana na uharibifu wa mazingira.

Mradi wa EBARR unatarajiwa kunufaisha zaidi ya kaya 29,000 na unakadiriwa kufikia wanufaika zaidi ya milioni moja kupitia utekelezaji shughuli za miradi mbalimbali kama vile upatikanaji maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kilimo na ufugaji, shughuli mbadala za kujiongezea kipato na urejeshaji vyanzo vya maji.

Unatekelezwa pia katika halmashauri za wilaya zingine za Mvomero (Morogoro), Simanjiro (Manyara), Kishapu (Shinyanga) na kwa upande wa Tanzania Zanzibar ni Kaskazini 'A'.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Agizo la RC Senyamule linapaswa kuungwa mkono na wakuu wa mikoa*

**MAGONJWA** ya kuambukiza kama vile maradhi ya moyo, shinikizo la juu la damu, figo na kisukari, yamekuwa yakiongezeka kila mwaka, hivyo kusababisha watu wengi kupoteza maisha. Sababu kubwa ambayo imekuwa ikitolewa na wataalamu wa afya ni mtindo wa maisha kutokana na watu kula vyakula vyenye wanga na mafuta kwa wingi, unywaji wa pombe uliopitiliza na kutokufanya mazoezi.

Ni kweli kwamba kutokana na mtindo wa maisha, watu wamekuwa wakitumia muda mwingi kukaa kwenye viti ofisini au nyumbani bila kujishughulisha na kazi za kuwafanya hata kutoa jasho.

Mtu anayefanya kazi ofisini, kwa mfano, akitoka nyumbani anaingia kwenye gari hadi kazini na akifika atatumia saa nane au zaidi akiwa amekaa kwenye kiti. Akishamaliza kazi, atapanda gari hadi nyumbani na akishafika atakaa kwenye kiti akipumzika na baadaye kula chakula kisha anakwenda kitandani.

Hata watoto, hususan wanaosoma shule za mchepuo wa Kiingereza, ambazo wazazi wenye uwezo wa kati na wa juu kiuchumi wanazoiona ndizo bora, wamekuwa na mfumo wa namna hiyo. Wanachukuliwa asubuhi kwa magari kutoka nyumbani kwenda shuleni na kisha kurudishwa nyumbani wakiwa kwenye mabasi ya shule.

Huo ndio mfumo mzima wa maisha wa miaka mingi kwa watu wengi hasa waishio kwenye miji mbalimbali. Matokeo yake ni kukumbwa na maradhi ambayo yanasababisha afya kuzorota na kutumia fedha nyingi kwa ajili ya matibabu na hatimaye kupoteza maisha.

Kutokana na kasi ya kuenea kwa maradhi hayo ambayo huathiri kwa kiasi kikubwa nguvu kazi ya taifa, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, ameibuka na wazo ambalo amelifanya kuwa agizo kwa wanafunzi wa shule zote mkoani humo kuanza kukimbia mchakamchaka kabla ya kuanza masomo ili kuwaweka katika hali nzuri ya kiafya. Zaidi ya hayo, amesema hali hiyo itawafanya vijana kuwa na afya, ukakamavu na uzalendo hatimaye kuwaepusha na maradhi yasiyo ya kuambukiza.

Akitoa kauli hiyo wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Wadau wa Elimu juzi, Senyamule aliweka bayana kwamba hakuna mwanafunzi anayeweza kufanya vizuri kwenye masomo kama hayuko vizuri kiafya. Ili kumfanya awe timamu katika afya na hatimaye kufanya vizuri katika masomo, mkuu huyo wa mkoa alisisitiza kuwa mazoezi ndiyo njia pekee.

Sambamba na kuwa katika afya njema, Senyamule alisema mchakamchaka utawafanya wanafunzi kuwa wazalendo pia kutokana na nyimbo watakazokuwa wanaziimba kwenye mazoezi hayo ya kuchangamsha mwili ili kuwaweka tumamu kiafya na kufanya vizuri katika masomo.

Kwa hakika jambo hilo limeungwa mkono na baadhi ya wakazi wa mkoa wa Dodoma waliohojiwa na gazeti hili kwamba hali hiyo itawawezesha vijana kuwa wakakamavu na kuamsha ari ya kujitambua na kufanya mambo mazuri kimaisha, ikiwamo masomo.

Kitendo cha kubuni na kuagiza wanafunzi wakimbie mchakamchaka asubuhi kabla ya masomo ni cha kupongezwa na kinaonyesha kiongozi huyo kuwa mbunifu na mwenye kutambua wajibu wake na anayeangalia mambo kwa mawanda mapana.

Ni ukweli ulio wazi kwamba afya ni suala la msingi katika maisha ya mwanadamu kwa kuwa mtu akiwa timamu kimwili, ana uwezo wa kufanya mambo vizuri tofauti na yule ambaye hayuko vizuri katika eneo hilo. Matokeo yake, hata hali za kimaisha baina ya watu hao ni lazima zitakuwa tofauti.

Mchakamchaka ulikuwa jambo la msingi kabla ya miaka ya 2000 kwa kuwa ilikuwa lazima kila mwanafunzi mwenye utimamu wa mwili akimbie na aliyeshindwa kufanya hivyo alichukuliwa hatua ama kwa kuchapwa viboko au kupewa adhabu ya kufanya usafi kwa muda fulani.

Hata afya za wanafunzi kwa wakati huo zilikuwa imara na kizazi hicho kilijitambua tofauti na sasa. Kongole RC Senyamule, viongozi wengine waige jambo hilo kwa manufaa ya afya za nguvu kazi ijayo ya Watanzania.






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# *Kupungua vifo Ukimwi, kifua kikuu, malaria, tujipongeze, tusishangilie*

**NI** kweli kabisa hata kwa macho tu na utafiti usio wa kitaalamu, inaonekana kuwa vifo vya magonjwa ya malaria, Ukimwi na kifua kikuu maarufu TB vimepungua.

Ni kwa sababu hata wagonjwa wake wamepungua sana. Sasa hivi hata mitaani kunyoosheana vidole kwamba, 'yule anao', hakuna tena.

Miaka ya nyuma tulikuwa na ndugu, rafiki na jamaa ambao baadhi walikuwa wakiugua ya ukiulizia utaambiwa ana maambukizo ya ugonjwa wa ukimwi, ingawa haisemwi hadharani.

Watu tumeunguza sana ndugu, rafiki na jamaa zetu na tumezika sana. Kwa sasa unaweza kukaa kwa muda mrefu kukawa hakuna ndugu, jamaa au rafiki ambaye ukaambiwa ana tatizo hilo.

Hiyo ni kuthibitisha kuwa maambukizi ya ugonjwa wa Ukimwi yamepungua. Kwa mujibu wa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu ni kwamba ugonjwa wa Ukimwi uliua watu 25, 000 mwaka 2021, lakini idadi ilipungua hadi kufikia 22,000 mwaka 2023.

Waziri huyo alitoa takwimu hizo akielezea miaka mitatu ya kuwa madarakani, Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwa upande wa malara, alisema 2021, iliua watu 1,882, lakini 2023 walipungua hadi, 1,540, wakati kifua kikuu 2023 kiliua watu 18,000, ukilinganisha na wagonjwa 26,800 waliokufa, 2023.

Kuna takwimu na uhalisia wa ndani ya jamii. Kama ilivyo kwa Ukimwi unaoonekana kwa sasa umepungua, hivyo hivyo kwa malaria na kifua kikuu.

Sasa unaweza kukaa hata mwaka mzima, hujasikia ndugu, jamaa au rafiki siyo tu amekufa kwa kifua kikuu, bali hata kuugua.

Miaka ya nyuma ilikuwa ni jambo la kawaida, kukuta ndani ya jamii kuna wagonjwa kibao wa kifua kikuu.

Nimeshuhudia jirani yangu akiwa anakwenda kumchukulia ndugu yake dawa Hospitali ya Mwanyamala, Dar es Salaam, ambaye alikuwa hawezi hata kunyanyuka kitandani, akiwa amedhohofu kwa kutafunwa na kifua kikuu.

**Sasa unaweza kukaa hata mwaka mzima, hujasikia ndugu, jamaa au rafiki siyo tu amekufa kwa kifua kikuu, bali hata kuugua.**

Mwezi mmoja tu baada ya kunywa dawa, hali ya mgonjwa ikawa vizuri akainukia na kuanza mwenyewe kwenda kunywa au kuchukua dawa.

Mara ya pili tena nikashuhudia mtoto mdogo tu, mwenye miaka saba akiwa anaumwa ugonjwa huo, ingawa naye baadaye alipona baada ya kunywa dawa.

Hiyo inakuonyesha kuwa magonjwa hayo yalikuwa tishio mno miaka kadhaa nyuma, lakini tunaishukuru serikali kuwa inapungua kila miaka inavyozidi kusonga mbele.

Sasa hivi ndani ya familia, ndugu jamaa, ukisikia mgonjwa amelazwa, basi kaanguka na bodaboda, ajali ya gari, presha, sukari, kiharusi, na hata vifo chanzo ni hayo au mengine yanayofanana hayo na mengi ni yale yasiyo ya kuambukiza.

Na hii imetahadharishwa pia na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, juu ya ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza, akisema tathmini inaonyesha mpaka kufikia mwaka 2030, nchi za Afrika, kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwamo Tanzania, zitakuwa zimekumbwa na magonjwa hayo kwa asilimia 70.

Tunamshukuru Rais Samia kwa kusimamia vyema sekta ya afya kiasi cha kila mwaka wagonjwa wanapungua na inawezekana huko mbele wakapungua zaidi, au kumalizika kabisa.

Hata hivyo, wakati serikali ikifanya kazi yake, wananchi wakati wakijipongeza kwa familia zao kuwa salama, lakini wasishangilie kupitiliza, badala yake wasiiachie serikali mzigo wote.

Umakini uendelee kuongezeka, watu waache ngono zembe, watumie vifaa kama kondomu ili kutoeneza magonjwa ya zinaa, waendelee kufyeka nyasi ndefu na kuweka mazingira safi ili kupunguza ugonjwa na vifo vinavyotokana na malaria.

Madirisha makubwa yenye mwanga yanayoingiza hewa safi, kutokukaa sehemu zenye mkusanyiko wa watu wengi bila sababu maalum, kunaepusha uwezekano wa kupata ugonjwa wa TB.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo na Kati wa Benki ya KCB Tanzania, Abdul Juma (aliyepiga magoti), akipiga makofi pamoja na viongozi mbalimbali, baada ya shughuli ya upandaji miti katika Msitu wa Pugu Kazimzumbwi, mkoani Pwani juzi. Miti 300 ilipandwa ili kusaidia uhifadhi wa mazingira kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# DC, dereva wake wapata ajali, wananchi wavunja kioo kuwaokoa

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Wilaya ya Musoma, mkoani Mara, Dk. Khalfan Haule na dereva wake, Robert Andrea, wamenusurika kifo baada ya gari kupasuka tairi ya mbele na kupinduka katika Kijiji cha Kwikuba, wikayani humo.

Akizungumza na Nipashe, Dk. Haule alisema ajali hiyo ilitokea juzi saa nane mchana wakati akitoka kukagua miradi ya maendeleo katika Kijiji cha Busekera.

"Tulikuwa tunarudi mjini Musoma, lakini isivyo bahati tairi ya mbele (kushoto) ikapasuka, gari likapinduka, lakini tunamshukuru Mungu ametunusuru na kifo. Ajali ilikuwa mbaya," alisema Dk. Haule.

Mkuu wa Wilaya alisema yeye na dereva wake walipata majeraha madogo ambayo yalitokana na kukatwa na vioo vya gari hiyo lenye namba za usajili STM 2744.

"Ninawashukuru wakazi wa Kijiji cha Kwikuba kwa jinsi walivyoguswa na tukio hili, walifika haraka eneo la ajali na kuvunja kioo cha juu cha gari, mmoja akaingia ndani na kukata mikanda na kututoa," alisema.

Dk. Haule alisema ingawa imekuwa ni kawaida kwa baadhi ya watu kufika kwenye ajali na kupora vitu, kwa wakazi wa kijiji hicho ni tofauti. Hawakupora chochote, badala yake walisaidia kuwaokoa.

Alisema wakazi wengi wa wilaya hiyo wanamfahamu, lakini anafafanua kuwa inapotokea ajali wanaweza kuwapo aliowaita wahuni, hata kama wanamfahamu wakaamua kufanya vitendo visivyo vya kiutu.

Dk. Haule alisema wakazi hao wameonesha utu, akiwashukuru kwa utu wao walioonesha katika tukio hilo la ghafla walilokumbana nalo.

"Baadaye lilikuja gari lingine la ofisi na kutuchukua, na leo niko katika Hospitali ya Mkoa wa Mara kwa ajili ya kuchunguza afya baada ya kupata michubuko kwenye sehemu mbalimbali za mwili," alisema.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Elias Magoma, alisema wakati ajali inatokea alikuwa dukani kwake; alisikia kishindo, alipotoka, akaona gari imeanguka.

"Kila mmoja alitoka na kukimbilia kwenye eneo la tukio, tulikuta DC na dereva wamo ndani, dereva akatuambia tuvunje kioo cha juu, tukafanya hivyo wakatoka ndani," alisema Magoma.

# Bil. 44/- zatumika kupeleka umeme vijijini

**Na Christina Haule,** CHALINZE

ZAIDI ya Sh. bilioni 44.146 zimetumika kutekeleza miradi ya umeme inayotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) mkoani Pwani na kufanikisha kuunganishwa umeme katika vijiji 107 kati ya 110 vilivyopo kupitia miradi mitatu ya umeme vijijini inayoendelea kutekelezwa.

Mkurugenzi Mkuu wa REA, Hassan Saidy alibainisha hayo jana mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge la Nishati ilipotembelea kijiji cha Tukamisasa kilichoko Tarafa ya Ubena Zomozi, Halmashauri ya Chalinze, mkoani Pwani kujionea maendeleo ya mradi wa REA awamu ya III mzunguko wa II.

Saidy alisema vijiji vilivyounganishwa umeme ni sawa na asilimia 97.3, vijiji vitatu pekee ndivyo vimebaki vikiwa katika maeneo ya Delta ya Rufiji, akiahidi vitafikishiwa huduma hivyo hivi karibuni.

"Vijiji vitano kati ya 10 vilivyomo katika maeneo ya Delta ya Rufiji vimetambuliwa kuwa vinapitika kwa njia ya barabara za msimu na vinaweza kuunganishwa umeme wa gridi, mkandarasi yuko maeneo ya mradi ili kufanya tathmini ya njia ya kusambaza miundombinu ya umeme katika vijiji hivyo, kazi ambayo inatarajiwa kukamilishwa kabla ya tarehe 30 mwezi Juni mwaka huu," alisema.

Alisema tayari mkandarasi wa fungu 23 anayetekeleza kazi katika mkoa wa Pwani M/s China Railway Constrution Electrification Bureau Group (CRCEBG) ameshatekeleza mradi kwa wastani wa asilimia 99.5 huku akitarajiwa kukamilisha kazi za mradi Machi 31, mwaka huu.

Saidy alisema mradi pia umelenga kupeleka umeme katika migodi midogo 30 iliyoko kwenye halmashauri za Bagamoyo, Chalinze na Kisarawe pamoja na maeneo ya kilimo ambayo hayajafikiwa na umeme mkoani Pwani kwa gharama zaidi ya Sh. bilioni 2.456.

Alisema mradi wa aina hiyo pia unatekelezwa mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 20.332.

Alisema kazi ya kupeleka umeme katika Kijiji cha Tukamisasa kilichoko wilayani Chalinze ilihusisha ujenzi wa njia za umeme msongo wa kati kwa kilomita 10.6, kilomita 3.3 za njia ya msongo mdogo na kufunga mashine kazi ambazo zimekamilika kwa asilimia 100 na tayari wateja 23 kati ya 66 wameshapatiwa umeme kwa zaidi ya Sh. milioni 466.

Hata hivyo, alisema tangu REA kuanzishwa mwaka 2007, jumla ya vijiji 11,843 vina umeme nchini ambavyo ni sawa na asilimia 96 ambapo vijiji 475 vitafikiwa hadi ifikapo mwezi Juni mwaka huu.

Saidy pia aliahidi kusimamia utoaji elimu kwa wananchi wa mkoa wa Pwani ili kuona umuhimu wa kupata huduma ya umeme kwenye maeneo yao na kuhakikisha matumizi ya umeme yanakuwa makubwa tofauti na mwitikio mdogo uliopo kwa sasa.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga alisema serikali inafanya mapitio ili kuona haki za wananchi zinakuwa sawa katika upatikanaji umeme kulingana na wakazi wa vijijini, vijiji miji na mijini ambao wanatofautiana katika malipo ya kuingiza umeme na kufanya wananchi kukosa uelewa.

"Kwa mradi wa REA, serikali hulipa kodi zote kwa asilimia 100 kwa kila mteja na hivyo mteja kulipia Sh. 27,100 tu kuingiza umeme ambayo ni kodi ya asilimia 18 ya Sh. 150,000 aliyopaswa kulipa, lakini kwa malipo ya wateja wa vijiji miji na mijini hulipa wenyewe gharama zote za Sh. 320,000," alisema Kapinga.

Alisema mapitio hayo yatasaidia pia kuendelea kutolewa elimu na jamii ili kuongeza uelewa na kufanikisha kuongezeka mwitikio wa matumizi ya umeme nchini.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Dk. James Mataragio, alitoa rai kwa wananchi kuchukua fursa iliyoko mbele yao kwa sasa kuunganishiwa umeme kwa bei ya chini na kuingiza umeme kwenye maeneo yao.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge la Nishati, Dk. Mathayo David alishauri wakazi wa vijijini kuona umuhimu wa matumizi ya nishati ya umeme kwa maendeleo kwa kuuza kuku wawili na kupata fedha za kuingiza umeme badala ya kusema wanakosa fedha za kuingiza umeme waliosogezewa na serikali.

Shabani Tungo, mkazi wa kijiji hicho alishukuru serikali kwa kuwafikishia huduma ya umeme ambayo inaonekana kurahisisha utekelezaji shughuli zao za maendeleo hasa kwa vijana kwa kufungua biashara mbalimbali za kuwaingizia kipato ikiwamo saluni za kike na za kiume na mashine za kusaga nafaka.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Mabadiliko tabianchi yaathiri mwalo wa Kibirizi, wafanyabiashara walia hasara

**Adela Madyane,** KIGOMA

WANAWAKE wafanyabiashara wa samaki na dagaa mkoani Kigoma wameiomba serikali kuboresha eneo la soko katika mwalo wa Kibirizi kutokana na eneo hilo kujaa maji yaliyosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Wamesema mvua inayoendelea kunyesha imesababisha kujaa maji kwa mwalo huo uliopo Manispaa ya Kigoma/ Ujiji na kuharibu miundombinu ya soko na kuhamishwa kutoka katika eneo hilo kupelekwa sehemu nyingine hali inayokwamisha shughuli za biashara.

Miongoni mwa masoko walikohamishiwa ni eneo la pembezoni mwa mwalo wa Kibirizi, kilomita mbili kutoka lilipokuwa soko la awali, soko jipya lililoanzishwa maeneo ya machinjio ya Kibirizi na soko la Gungu.

Mmoja wa wafanyabiashara wa samaki wabichi, Mariam Shaban, alisema kipato chake kimeshuka kutokana na kuhamishwa na samaki wanaharibika kwa kukaa muda mrefu bila kuuza.

"Nilikuwa nauza zaidi ya elfu 20 kwa siku, ila sasa nauza elfu tatu kwa siku, hali ya maisha yangu imebadilika ghafla, serikali itutengee eneo maalumu la soko linalofikika kwa urahisi, huku ni mbali, wateja hawafiki na mboga zinaharibika, tutawalejee watoto wetu," alilalamika Shaban.

Hassan Juma, alisema serikali inapaswa kuchukua hatua za haraka kuboresha miundombinu ya soko au kutenga eneo maalumu la soko kwasababu tatizo la kujaa maji katika eneo hilo inakwamisha shughuli za biashara na kuathiri upatikanaji wa kipato cha kila siku.

Aidha, Fatuma Rashid alisema eneo walilopo ni la mtu binafsi, mwenye eneo lake anaweza kubadili mawazo na kuwaondoa.

Msafirishaji wa mizigo na abiria kwenda maeneo ya mwambao mwa Ziwa Tanganyika, Issa Mustapha, alisema kutokana na mabadiliko ya tabianchi na mvua zinazoendelea kunyesha ni muhimu serikali ikaongeza nguvu kuboresha bandari hiyo.

"Gati limejaa maji na inatulazimu kutembea na mizigo mita kadhaa tukiwa tumeibeba ndani ya maji ili kuingiza ndani ya boti hali hii inaweza kusababisha hasara kwa wenye mizigo endapo itadondoka kwenye maji wakati wa kubeba," alitahadharisha Mustapha.

Kaimu Ofisa Biashara wa Manispaa ya Kigoma Ujiji, Kanyama Kalombo, alisema wanaendelea na mchakato wa kuwaandalia wafanyabiashara hao maeneo ya soko ya kufanya biashara zao kwa muda na watafanya kwa uhuru na kuendelea kuingiza kipato chao kama kawaida.

Meneja wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) Kigoma, Silvester Mabula, alisema wanajipanga kufanya tathmini na kuangalia njia mbadala ili wateja wao na wananchi waweze kuendelea kupata huduma za usafiri na usafirishaji kama awali.

"Kutokana na kujaa maji TPA haijakaa kimya inaangalia njia mbadala kuhakikisha huduma za wateja zinaendelea kufanyika kama kawaida na tunafanya tathmini ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya kuangalia upande mwingine wa bandari hiyo kwa ajili ya kutengeneza njia nyingine ambayo wataitumia wateja wetu kwani eneo hili ni muhimu sana kwetu," alisema Mabula.

Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Salum Kalli, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari ya mvua na kuwataka wafanyabiashara wa samaki na dagaa kuhama kwa muda kutokana na maji kuongezeka katika eneo lao la biashara.

Alisema hakuna sababu ya wafanyabiashara hao kupanga biashara zao barabarani kwa kuwa masoko yapo ya kutosha kwa ajili ya kufanyabiashara.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, wakikagua maendeleo ya ujenzi wa hoteli katika mradi unaosimamia na NSSF. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WMA yaanza kuhakiki mita za umeme

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Vipimo (WMA), imeanza kazi ya kuhakiki mita za umeme ili kuwa na usawa kwenye matumizi sahihi ya vipimo kama inavyoelekeza Sheria ya Vipimo.

Kuanzia sasa mita zote mpya za umeme hazitafungwa kwa wateja kabla ya kufanyiwa uhakiki na WMA na katika awamu ya kwanza, wakala imepokea mita 500 kupitia kituo chake cha uhakiki wa vipimo kilichoko Misugusugu Mkoa wa Pwani.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stella Kahwa, alisema jana kuwa mita 500 zimepokewa kutoka kampuni ya CRJE (East Africa) Ltd., ambayo imepata kazi ya kusambaza mita hizo ambazo zinatarajiwa kwenda kufungwa katika mradi wa REA mkoani Geita.

Kahwa alisema uhakiki wa mita hizo za umeme umefanyika kwa muda wa siku moja na mteja kukabidhiwa mita zake.

Pia, alisema wakala ina uwezo wa kupima mita nyingi za umeme kwa kutumia muda mfupi kwa kuwa ina mitambo ya kisasa na miwili iko katika kituo cha uhakiki wa vipimo Misugusugu na mmoja upo katika jengo la WMA mkoani Kilimanjaro. Alisema katika mita 500 zilizowasilishwa, asilimia 95 zimepita kwenye uhakiki na zimewekewa rakili (seal) kwa ajili ya kuzilinda zisichezewe na asilimia tano ya mita hazijaruhusiwa kuingia katika matumizi mpaka zitakapofanyiwa marekebisho na kuletwa tena kuhakikiwa na endapo zitakidhi vigezo zitaruhusiwa kutumika.

"Wakala wa Vipimo inaendelea kutoa wito kwa wadau wanaopata zabuni za kusambaza mita za umeme kuhakikisha mita zao zinaletwa WMA kwa ajili ya uhakiki ili kujiridhisha kama zinapima kwa usahihi kama Sheria ya Vipimo Sura Na. 340 inavyoelekeza," alisema na kuongeza.

"Lengo hapa ni kuhakikisha mteja anapata vipimo sahihi katika mita na Shirika la Umeme (TANESCO), linakusanya fedha kulingana na matumizi sahihi ya umeme yanayotumiwa na wateja wao kwa hiyo kupitia kazi hii ya uhakiki mteja atakuwa na uhakika zaidi kwamba analipa kile anachotumia," alisema.

Kituo cha WMA Misugusugu kinapima ujazo sahihi wa matangi ya magari ya mafuta, upimaji wa mita za maji na sasa mita za umeme.

Alipotembelea kituo hicho mwaka juzi, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema serikali imenunua mtambo kwa Sh. milioni 500 na mita zote za maji hupimwa kabla ya kufungwa.

Alisema hali hiyo imesaidia kuondoa malalamiko ya wananchi ambao hulalamikia mita ambazo huwapunja maji wanapofungiwa.

"Malalamiko kwamba mita za maji wanazofungiwa ni feki yalikuwa mengi mno sasa kupitia mtambo ule tunakuwa na uhakika kwamba mita inayokwenda kufungwa kwa mteja na taasisi zingine zinakuwa sahihi kwasababu zinasoma vipimo sahihi," alisema.

# Kamati ya Bunge yafurahishwa Rais Samia kuruhusu mradi hoteli nyota 5

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, imefurahishwa na hatua ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuruhusu kuendelea na ujenzi wa miradi mikubwa ya kimkakati, ikiwamo inayotekelezwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatuma Toufiq, alisema hayo wakati wajumbe wa kamati hiyo walipofanya ziara ya kutembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa hoteli ya nyota tano inayomilikiwa na NSSF iliyopo jijini Mwanza, Machi 18, 2024.

"Nimpongeze sana Rais, Dk. Samia, mradi huu ulikuwa umesimama kwa muda mrefu, lakini alipoutembelea mwezi Juni 2023, aliwatia moyo na kuwataka NSSF waendelee, akijua utakuwa na tija kwa wananchi wa Mwanza na mikoa ya jirani na kuongeza mapato kwa serikali," alisema Fatuma.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo akiwamo Neema Mwandabila, alimpongeza Rais kwa uamuzi wake wa kuruhusu miradi iliyosimama iendelee kutekelezwa. Aidha, ameipongeza NSSF kwa ujenzi wa mradi huo kwa kuwa Mkoa wa Mwanza unauhitaji wa hoteli ya aina hiyo.

Naye Mwita Getere, alisema NSSF ina nidhamu katika kutekeleza miradi ya uwekezaji ukiwamo wa hoteli ya nyota tano iliyopo jijini Mwanza.

Mariam Kisangi, alisema mradi huo wa hoteli utaleta manufaa kwa NSSF, jamii na Taifa kwa ujumla.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Profesa Joyce Ndalichako, alimshukuru Rais Samia kwa kuridhia mradi huo uendelee baada ya kusimama kwa muda mrefu.

Alisema mradi huo ulianza Novemba mosi, 2013 na ulipangwa ukamilike ndani ya miaka mitatu, lakini kutokana na changamoto mbalimbali, utakamilika Desemba 30, 2024.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, aliwashukuru wajumbe wa kamati hiyo kwa maoni na michango yao ambayo wataenda kuyafanyia kazi.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema kuna mpango wa kuboresha uwanja wa ndege wa Mwanza ili iwe rahisi watalii kupita kwa wingi na kuiwezesha hoteli hiyo kupata wageni wengi.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, alisema Mfuko unaendelea kutekeleza majukumu yake mbalimbali, kwa upande wa ulipaji wa mafao ya wanachama, wanalipa kiasi kikubwa zaidi ya kile ambacho mwanachama amechangia na ndio maana wanafanya uwekezaji wenye tija.





## Mifugo inayoharibu miti kutaifishwa

**Na Ashton Balaigwa,** SAME

SERIKALI imeamuru kukamatwa na kutaifishwa mifugo inayoharibu na kula miti inayopandwa katika kampeni za kitaifa ili kurejesha uoto wa asili maeneo yaliyopewa kipaumbele.

Amri hiyo ilitangazwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, wakati akizindua Maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na Siku ya Upandaji Miti inayofanyika kitaifa wilayani hapa.

"Hapa nataka wakuu wa wilaya zote wanisikilize kwa makini sana, mifugo yote inayobainika kufanya uharibifu kwenye miti iliyopandwa na Serikali na wadau katika kampeni za upandaji miti, kuanzia sasa itaifishwe na kuwa mali ya umma," alisema na kusisitiza kuwa:

"Serikali hatuwezi kupanda miti halafu wafugaji wafanye kuwa sehemu ya malisho."

Babu aliwaagiza maofisa ardhi nchini kutotoa kibali cha ujenzi kwa waliopewa viwanja, kabla ya mmiliki kupanda miti mitano ikiwamo ya matunda katika kiwanja chake.

Alisema amelazimika kutoa agizo hilo kwa wakuu wa wilaya zote nchini kutokana na tukio la hivi karibuni, ambalo aliongoza upandaji miti 7,000 eneo la Chekereni, baada ya siku chache ililiwa na mingine kuharibiwa na mifugo.

"Maadhimisho hayo ya kitaifa tumeyafanyia Wilaya ya Same kwa sababu nyie wote mnajua tunapotoka Moshi kwenda Dar es Salaam au kutoka Dar es Salaam kwenda Moshi mnaona hali ya Same ilivyokuwa sio ya kuridhisha. Tumeamua kupanda miti ya kutosha kurudisha Same ya kijani" alisema Babu.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Same, Kasilda Mgeni, alisema katika kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan, wilaya hiyo imepanda zaidi ya miti 500,000 kandakando ya barabara kuu,maeneo ya wazi,ofisi za Serikali na shule zote ili kurudisha uoto wa asili.

Kasilda, alisema ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kutekeleza agizo la mkuu huyo wa Mkoa wa Kilimanjaro, watahakikisha wanaendelea kutunza hifadhi za mazingira katika maeneo yote ikiwa pamoja na kuweka sheria kudhibiti uharibifu.

"Katika wilaya ya Same tayari tumeshatii agizo lako mkuu wa mkoa kwani tumeshapanda miti kandakando ya barabara kuanzia mwanzo wa wilaya hadi mwisho wa wilaya yetu na inatunzwa vizuri," alisema Kasilda.

# Wanakijiji walilia fidia kwa Silaa

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

ZAIDI ya wakazi 370 wa Kijiji cha Oldonyo Sambu Wilaya ya Arumeru mkoani hapa, wamewasilisha malalamiko yao kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa kwa kuchukuliwa ardhi yao bila kulipwa fidia.

Diwani wa Kata ya Oldonyo Sambu, Raymond Lairumbe, aliwasilisha malalamiko hayo kwa niaba ya wakazi hao jana kwa Waziri Silaa, ambaye yuko jijini Arusha kusikiliza malalamiko ya wananchi kupitia kliniki ya ardhi ili kutatua migogoro ya ardhi.

"Baada ya kuchukuliwa ardhi hii, wakazi wa eneo hili, tulitakiwa kuhamia eneo jingine la Bwawani tulilopewa na Serikali, lakini tulipoenda huko mwaka 2015 tulikutana na wavamizi walitufukuza wakidai eneo lina mwekezaji," alisema.

Alisema wakazi hao wa kata yake, wanaendelea kuteseka, hawana maeneo ya makaburi wala kilimo kwa ajili ya mazao ya chakula.

"Baada ya eneo letu kuchukuliwa na kufikisha kilio chetu kwa Waziri Mkuu (wakati huo), Fredrick Sumaye. Tukiwa na nyaraka zetu za Novemba mwaka 1994, alimuagiza Mkuu wa Mkoa wa Arusha wa wakati huo, Mohamed Babu kuwatunza wananchi hao na kuwapa chakula hadi serikali itakapowapatia eneo lingine," alisema.

Alisema mwaka 2021, waliokutana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (wakati huo), William Lukuvi, akiwa katika ziara yake Halmshauri ya Arusha kwa ajili ya kutatua kero za ardhi.

"Huyu naye alituahidi kutupatia eneo la Bwawani ambalo toka mwaka 2015 lina mgogoro baada ya mwekezaji kulimiliki ila taratibu za mahakama zilifanyika na mwaka juzi shamba likakabidhiwa mikononi mwa halmashauri hii baada ya serikali kulipa fidia ya Shilingi bilioni 5.7," alisema diwani huyo.

Alisema mchakato wa kuligawa shamba hilo ukaanza bila kupewa kipaumbele wakazi hao na mwaka jana, aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo, Anjelina Mabula alifika eneo hilo na kudai wakazi wa Oldonyo Sambu ni wengi, walilipwa fidia na hawapo.

Kiongozi wa kimila (Laigwanani) wa eneo la Seuli, Sindio Kassim, alisema wakazi hao wananyanyaswa na serikali, hivyo wamefika kwa Waziri Silaa wakiamini atawashughulikia na endapo akishindwa kama watangulizi wake, watahama.

Akijibu kilio hicho, Waziri Silaa, aliomba kukutana na kiongozi wao mwishoni mwa wiki ili kutengeneza utaratibu mzuri wa kutatua mgogoro huo.

"Mimi leo ndio nalisikia hili kwa mara ya kwanza na mkuu wa mkoa huu hayupo yupo Dodoma kuna vikao vya bajeti vinaendelea, naombeni mnivumilie tutafikishana mahali pazuri nikiwa na wawakilishi wenu," alisema.




Katibu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, akipanda mti wa matunda kama ishara ya ufunguzi wa Benki ya Vinasaba vya mbegu asili za mbogamboga na matunda, jijini Arusha jana. Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Emmanuela Kaganda na Mkurugenzi wa Afrika wa Taasisi ya World Vegetable, Dk. Gabriel Rugalema. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Benki kuhifadhi mbegu miaka 100 nchini

**Na Daniel Sabuni,** ARUMERU

TAASISI ya Utafiti wa Vinasaba na Uendelezaji wa Mbegu Asili za Mboga na Matunda imezindua benki ya kuhifadhi mbegu za mboga na matunda kwa kipindi cha miaka 100 bila ya kuathirika na kutumika katika kilimo.

Akizindua benki hiyo jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Mweri, alionya isitumike kama makumbusho ya taifa na kufungia mbegu bali zisambazwe ili kusaidia kuboresha lishe bora kwa wananchi.

"Kuwapo kwake hapa kuwe na tija kwa wakulima na maduka ya mbegu. Mbegu zikitafitiwa na kuhifadhiwa vizuri, hustahimili ukame, kupambana na magonjwa na kupata mazao mengi," alisema Mweri na kuongeza kuwa:

"Serikali iko tayari kutoa ushirikiano utakaohitajika ili malengo tarajiwa ya World Veg yafikiwe. Kuwapo Tanzania kwa benki hii ni bahati ya pekee kabisa kwa sababu itasaidia vijana na wanawake kujiajiri kwenye mashamba ya bustani na hatimaye kujipatia vipato na kupunguza umaskini."

Benki hiyo iliyojengwa katika Kijiji cha Tengeru, Wilaya ya Arumeru kwa gharama ya zaidi ya Shilingi bilioni 1.2 kwa ufadhili wa nchi za China na Uholanzi, itatumika kuhifadhi mbegu na kusambazwa kwa wakulima na kampuni ya mbegu barani Afrika.

Baadhi ya aina za mbegu zinazohifadhiwa katika benki hiyo ni mchicha lishe, bamia, ngongwe (nyanya chungu), mnafu, nyanya na vitunguu.

Mweri, alitaja moja ya changamoto ya dunia kwa sasa kuwa ni kushindwa kuhifadhi mbegu zikiwa na ubora ule ule wa vitamini na madini, hivyo kusababisha utapia mlo.

Katibu Mkuu huyo, alisema benki hiyo imehifadhi aina za mbegu 5,700 na mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka huu itakuwa na aina 11,000 za mbegu. Alisema malengo hadi kufikia mwaka 2025/26 itakuwa imehifadhi aina 25,000 za mbegu hizo.

Alisema kituo cha World Veg kilichoanzishwa mwaka 1992, kimemudu kuhifadhi mbegu za mboga na matunda kutoka 1997, na mpaka mwaka huu zina ubora ule ule.


Awali Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya World Veg Afrika, Dk. Gabriel Rugalema, alisema kuzinduliwa kwa benki hiyo kutapanua wigo wa uhamasishaji kwa wanasayansi wa dunia, kufanya utafiti zaidi na kupata ubora na mbegu nyingine.

"Wanasayansi wanaweza kuendelea zaidi ya hapa baada ya kuhifadhiwa mbegu kwenye benki na kupata faida zaidi na mavuno zaidi.

Alisema kituo hicho kimeiheshimisha Tanzania katika macho ya kimataifa, kutokana na umuhimu wake kwa Bara la Afrika na dunia yote.

Mkurugenzi huyo, alisema pia mbegu zilizohifadhiwa zinatumika kufundishia vikundi vya wanawake, vijana na wakulima katika mikoa mbalimbali nchini ili kuongeza ajira na kupata kipato cha kaya.

Alitaja aina ya nyanya inayofahamika kwa jina la Tengeru 97, iliyotafitiwa na kuhifadhiwa na World Veg inayotumika kwa mkoa wa Arusha na jirani kuwa inamudu kupambana na magonjwa, hali ya hewa na kuzaa mavuno mengi na bora.





# Neema bomba la mafuta Uganda hadi Tanga

**Na Waandishi Wetu**

KIWANDA cha kuweka mfumo wa kuhami joto katika bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Chongoyeni nchini Uganda hadi Hoima Tanga kinatarajia kuanza kazi mwezi ujao.

Kukamilika kwa kiwanda hicho kilichopo Kijiji cha Sojo Kata ya Ugusule Wilaya ya Nzega mkoani Tabora na kuzinduliwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko Machi 26 ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa mafuta ghafi kikiwa na uwezo wa kuweka mfumo wa joto katika mabomba yenye urefu wa kilomita 100 kila mwezi hali itakayosaidia mradi huo kukamilika kwa wakati.

Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo la Petroli Nchini (TPDC), Mussa Makame aliyasema hayo juzi wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge Hesabu za Serikali (PAC) ilipotembelea kiwanda hicho kukagua fedha zilizoidhinishwa na Bunge zinavyotumika.

Alisema ujenzi wake umefikia asilimia 61 na kitaanza kuweka mfumo wa joto kwenye bomba zitakazotumika kusafirisha mafuta ghafi ambazo mpaka sasa zipo tayari zikisubiri kukamilika kwake.

"Kwa sasa bomba zipo za kutosha na kazi iliyobaki ni kuzivisha mfumo wa kuhami joto tu ili zisiwe zinapoteza joto wakati wa usafirishaji wa mafuta ghafi hivyo muda siyo mrefu mwaka huu kitazinduliwa na Naibu Waziri Mkuu," alisema Makame.

Makamu Mwenyekiti wa PAC, Jafeti Hasunga, alisema kamati hiyo wameridhishwa na mwenendo wa ujenzi wa kiwanda hicho na thamani ya mradi unaonekana.

Alisema kuwepo kwa mradi huo kumesababisha Kata ya Sojo kupata maendeleo katika sekta ya afya, maji, elimu na miundombinu ya barabara baada ya waliopisha kulipwa fidia na fedha kuelekeza kwenye ujenzi wa nyumba bora za kisasa na kuondokana na kuishi kwenye nyumba za tope na nyasi.

"Sehemu zote nchini ambako mradi huu umepita wananchi waliotakiwa kupisha mradi walifidiwa maeneo yao kwa kupewa fedha au kujengewa nyumba za kisasa na sasa na baadhi yao wamepata ajira," alisema Hasunga.

Mratibu wa masuala ya Kijamii wa Mradi huo, Editha Ngaiza, alisema wamekuwa wakishirikisha wananchi, kuwapatia elimu ya ujasiriamali na namna ya kuandika barua za kuomba kazi na kuajiriwa.

**Imeandaliwa na Shaban Njia na Marco Maduhu, (NZEGA).**



Mmoja wa wanachama wa Chama cha Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA), Parokia ya Mugumu, wilayani Serengeti Mkoa wa Mara, Matilda Mathias (kushoto), akikabidhi msaada wa mfuko wa unga kwa Monica Maningu, mkazi wa Mugumu juzi, ikiwa ni utekelezaji wa tendo la huruma kwa wahitaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kiama waganga ramli chonganishi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MUUNGANO wa Waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala (TATDM) Mkoa wa Shinyanga umetangaza kiama dhidi ya waganga wanaojihusisha na ramli chonganishi ili kudhibiti mauaji ya watu wasiokuwa na hatia mkoani hapa.

Hatua hiyo imekuja baada ya kubaini vitendo hivyo vimekuwa vikizua hofu na husudani kwa watoto, wanawake na wazee wanaoishi maeneo ya uchimbaji madini.

Akizungumza kwenye kikao cha waganga wa tiba asilia mjini hapa juzi, Mwenyekiti wa TATDM, David Simlembe,

alisema kupitia muungano huo watalisaidia Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga kuwafichua waganga hao kwa kukiuka maadili ya kazi yao ili kudhibiti mauaji hayo kutokana na imani potofu.

"Ili tufanye kazi zetu za kuagua kwa kutii sheria za nchi na kuzingatia miiko na fani yetu, tutawafichua wale ambao sio waadilifu wanaopiga ramli chonganishi," alisisitiza.

Katibu Mwenezi wa Muungano huo mkoani hapa, Christopher Kubanda, aliwahimiza waganga wote kujisajili kwenye Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala na muungano huo ili watambulike kisheria.

Baadhi ya waganga hao, akiwamo Yusuph Shedafa, alisema kupitia muungano huo, watawabaini waganga matapeli na wanapiga ramli chonganishi.

Akizungumza na Nipashe Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alisema wamekuwa wakiwasaka waganga wanaopiga ramli chonganishi ili kudhibiti vitendo hivyo mkoani hapa licha ya kazi hiyo kuwa na changamoto.

Kamanda Magomi aliahidi kushirikiana na muungano huo na kuutaka kuwafichua waganga wasiokuwa waadilifu ili wakamatwe na kuchukuliwa hatua kali.

Alisema jeshi hilo litashirikiana na waganga hao kutokomeza mauaji yanayotokana na imani za kishirikina kwa kufanya msako mara kwa mara.

# Kampuni kuajiri 1,000 mgodini

**Na Timothy Itembe,** MARA

ZAIDI ya watu 1,400 mkoani hapa wanatarajia kupata ajira katika Mgodi wa Dhahabu wa Barrick North Mara kupitia kampuni 118 zinamilikiwa na wafanyabiashara wa maeneo jirani na mgodi huo.

Hayo yalisemwa juzi na Meneja Mkuu wa Mgodi huo, Apolinary Lyambiko, wakati wa kufunga mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyabiashara wazawa ya fursa za biashara katika maeneo ya mgodi na mengine.

Lyambiko, alisema hadi sasa mgodi huo, umesajili kampuni 118 za biashara ndani ya mgodi na kutoa ajira kwa watu hao 1,444 wengi wao kutoka maeneo yanayouzunguka. Mgodi huo unaendeshwa na Barrick kwa ubia na serikali kupitia Kampuni ya Twiga Minerals.

"Mfano kwa mwaka 2023 kampuni yetu imetoa Shilingi bilioni 96 ambazo zimelipwa kwa wazabuni wazawa kupitia falsafa ya utolewaji kipaumbele kwa wazawa. Jitihada hizi zimechangia kwenye ustawi wa maendeleo ya jamii na kuimarisha mahusiano yetu na jamii inayotuzunguka," alisema.

Alisema kampuni hizo ni alama muhimu kukuza biashara ya wazawa mkoani Mara kupitia programu ya maendeleo ya kibiashara ya Barrick.

Alisema programu hiyo inalenga kuimarisha uwezo wa biashara za ndani kunufaika na fursa zilizopo kwenye sekta ya madini ambayo imewafikia walimiki 19 wa kampuni za wafanyabiashara.

Meneja Ukaguzi wa Fedha, Kodi na Ushirikishwaji wa Watanzania kutoka Tume ya Madini, Annasia Kwayu, alisema mpango huo ni utekelezaji wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na kanuni za ushirikishwaji wa Watanzania za Mwaka 2018 na marekebisho yake.

Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Juma Chikoka, alisema programu hiyo imeendelea kuinua wafanyabiashara wa Mara ikiwa ni pamoja na wananchi kuendelea kupata ajira.

**"Mfano kwa mwaka 2023 kampuni yetu imetoa Shilingi bilioni 96 ambazo zimelipwa kwa wazabuni wazawa kupitia falsafa ya utolewaji kipaumbele kwa wazawa. Jitihada hizi zimechangia kwenye ustawi wa maendeleo ya jamii na kuimarisha mahusiano yetu na jamii inayotuzunguka," alisema.**

ama
ALHAMISI MACHI 21, 2024
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 13

## Rais Samia anavyodumu 'kumimina' pesa kwenye afya zao mama na mtoto




## MIAKA 3 YA RAIS & SIKU MISITU DUNIANI... Safari yake kwenye uwekezaji na kuendeleza hazina misitu ya Taifa

Ukurasa 12

### KONGAMANO LA KIMATAIFA WIKI JANA ...

# Samia aonyesha 'umama' alipotoa darasa mtoto alivyo na anavyolelewa

**Na Sabato Kasika**

WIKI iliyopita kulikuwapo kongamano kubwa la kimataifa la malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto lililofanyika mjini Dar es Salaam kwa siku nne,

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwaingiza darasani washiriki wa kongamano hilo tafsiri ya mama na malezi.

Ni kongamano lililoanza Machi 11 hadi 14 mwaka huu, likihusisha wadau zaidi ya 1000 kutoka nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na wengine kutoka nchi za Ulaya, Amerika na Asia huku yeye akiwa mgeni rasmi.

Katika hotuba yake iliyosomwa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, Rais anasema Afrika bado ina changamoto ya uwekezaji katika malezi.

Rais anafafanua kuwa utafiti mbalimbali uliofanyika barani Afrika mwaka uliopita, umebaini kuwapo tatizo la uwekezaji katika malezi na makuzi ya watoto wadogo.




Katika staili yake ya urafiki na watoto kwenye ukaguzi wa shughuli za afya kitaifa. **PICHA: MTANDAO.**

**JINSI ALIVYOTOA SOMO**

Rais Dk. Samia anasema, sayansi ya malezi na makuzi ya mtoto inaelekeza kuwa ubongo wa binadamu unakua na kufikia hadi asilimia 90 katika umri wa kutunga mimba akiwa tumboni mwa mama yake hadi miaka nane.

"Wataalamu wa afya wanaelekeza kuwa, ili kufikia kiwango hicho cha ukuaji, mtoto na mama wanatakiwa kupatiwa huduma bora za afya, lishe ya kutosha, huduma za awali za kumchangamsha mtoto, malezi yenye kuitikia hisia za mtoto na ulinzi na usalama wa mtoto," Rais anasema.

Pia anafafanua namna huduma hizo zinatakiwa kutolewa katika uwiano ulio sawa, kwa kuwa huduma zote hizo zina mchango unaofanana, katika ukuaji ubongo wa mtoto na kwamba utafiti unaonyesha uwiano huo haupo.

Rais anasema, hali hiyo ikiendelea bila kuchukuliwa hatua za kuwekeza katika malezi, mataifa ya Afrika yatakuwa yanaandaa watoto, ambao ni nguvu kazi isiyo na tija kwa mataifa yao.

Anaeleza anachokitamani ni kuona nchi za ukanda huo na sehemu nyingine zikiongeza uwekezaji katika huduma za malezi na makuzi ya watoto hasa maeneo ya afya, lishe, kujifunza na uchongamshaji wa awali, malezi ili kuwa na matokeo chanya.

"Ni muhimu wadau wote kujadili na kuja na mbinu bora zaidi za kuimarisha afua za malezi na makuzi ya watoto kwa kuzingatia mila na tamaduni zetu na kuepuka zenye madhara kama za ukeketaji," anasema Dk. Samia.

Anasema, jamii iliyostaarabika haipaendi kuona watoto wanafanyiwa vitendo vya ukatili, kwa kuwa malezi na makuzi ya watoto kwa sasa yanaathiriwa na changamoto mbalimbali zikiwamo migogoro ya familia, ambayo waathirika wakubwa ni watoto.

Inaendelea Uk. 13

MAZINGIRA

## MIAKA 3 YA RAIS & SIKU YA MISITU DUNIANI...

# Safari yake kwenye uwekezaji na kuendeleza hazina ya miti kitaifa

**Na Elizabeth Zaya**

SASA imetimu miaka mitatu ya taifa kuongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, tarehe kamili ikiwa juzi.

Ndani ya maadhimisho hayo, wanamisitu 'wanajambo loa' wakisherehekea Siku ya Misitu Duniani leo. Nao wako chini ya uratubu na usimamizi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Miongoni mwa wanaopigiwa makofi, ni Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) inayoweka wazi mafanikio yake katika hesabu, ina mchango wa uongozi wa rais huyo.

Katika hilo, TFS ina hesabu inayogusa makusanyo ya maduhuli ya Sh. 371,956,374,658.38, ikiwa ni mapato kutoka vyanzo vya ndani na kuwasilisha kwenye Ofisi ya Msajili wa Hazina Sh. 52,150,354,836. Hiyo ni asilimia 14 ya makusanyo.

Miongoni mwa mikakati inayotajwa kuwezesha mafanikio hayo ya kukusanya maduhuli hayo, ni pamoja na huduma za utalii, mazao ya misitu na vivutio vya utalii ikolojia, vilivyopo kwenye misitu hiyo.

Kwa mujibu wa TFS inayoongozwa na Kamishna wa Uhifadhi, Prof. Dos Santos Silayo, utalii na biashara ya mazao ya misitu na nyuki ni miongoni mwa vinavyochangia mapato yake.



Sehemu ya Misitu ya Sao Hill, mkoani Iringa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Mazao mengine ya misitu yanayowapatia kipato, yanatajwa ni uvunaji utomvu wa miti katika mashamba mbalimbali ya miti ikiwamo la Sao Hill, mkoani Iringa na uzalishaji wa gundi kutoka katika miti ya migunga.

Prof. Silayo anasema, kuna fursa zinazopatikana katika soko la bidhaa za nyuki na kwamba kila mwaka hupeleka sampuli 70 za asali katika maabara za kimataifa, ikiwamo Ujerumani kutoka katika wilaya zisizopungua 30, ambazo mara zote ubora wake umekuwa ukikidhi viwango vya kimataifa.

Anasema kutokana na ubora huo, asali ya Tanzania imeendelea kuvutia watu wengi, hivyo kupata soko kubwa la ndani na nje ya nchi.

Prof. Silayo anaelezea zaidi mafanikio ya wakala huyo katika kipindi hicho cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia, kuwa ni pamoja na kuanzisha misitu mipya 55 yenye ukubwa wa hekta 1,453,025.846 ambayo tayari ilishatangazwa kupitia Gazeti la Serikali (GN).

Kwamba wakala, tayari umeanzisha mashamba matatu ya nyuki yanayojulikana kama Nyuki Mwambao Bee Farm yenye hekta 2,412.76; maeneo ya Kondoa Manyoni, Bee Farm, hekta 7,469.8; na Kipembawe Bee Farm, lenye hekta 20,728, kwa ajili ya kuongeza uzalishaji mazao ya nyuki.

Katika eneo la uzalishaji, anasema imezalisha jumla ya miche 95,897,870 ambayo ilipandwa katika mashamba ya miti pamoja na kutolewa kwa jamii ambayo iliipanda katika maeneo mbalimbali nchini yaliyoharibika.

Prof. Silayo anasema, wakala umepanda miti eneo la mashamba lenye ukubwa wa hekta 18,292 kwa ajili ya kuzalisha rasilimali za viwanda vya misitu na kuanzisha shamba jipya katika hekta 37,000 wilayani Tunduru.

Mtazamo ni kwamba, kumekarabatiwa njia za kutembelea watalii zenye urefu wa kilomita 873, barabara za msituni kilomita 68 na kambi za kitalii 43.

Kadhalika, anasema wamejenga miundombinu mipya ikiwamo barabara za kilomita 82 na njia za kitalii kilomita 348, vituo vyote sita vya malikale navyo vimeboreshwa kwa kujenga maeneo ya kupumzikia.

Mengine anataja, ni ukarabati wa majengo na miundombinu kupitia Mpango wa Taifa wa kukabiliana na athari za UVIKO-19 na kwamba jumla ya 'malango' ya kisasa matano yamejengwa.

Vilevile kunatajwa kuwapo kilomita 96 za barabara za msituni na kilomita 190 za njia za watembea kwa miguu, msitu ukijengwa katika Hifadhi za Misitu ya Mazingira asilia 11.

Vivutio vya wakala, vimepokea watalii 488,336 wakiwamo wa ndani 426,400 na wageni 61, 936.

Inaelezwa, kuwapo jumla ya tani 70.6 za asali na tani 2.6 za nta zimezalishwa pamoja na kununua magari 52 na pikipiki 43, kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa taasisi katika kutekeleza majukumu yake.

Pia, Prof. Silayo anafafanua, wakala huo umejenga majengo 88, zikiwamo ofisi 33, nyumba za watumishi 29, vituo vya ulinzi 26 na maghala ya kuhifadhi silaha nane.

**MABORESHO YA MISITU**

Nyingine inatajwa ni usafishaji mipaka ya misitu yenye urefu wa kilomita 3,873.49, kuweka vigingi 3,045 na mabango 1,808, na kupanda miche 54,463 mipakani.




Kamishna wa Uhifadhi, Prof. Dos Santos Silayo.

Hadi sasa inatajwa TFS, imeandaa mipango ya usimamizi wa misitu 119 katika eneo lenye ukubwa wa hekta 2,539,095.04 ili kuimarisha usimamizi wa misitu.

Prof. Silayo anasema, TFS imeshapandisha hadhi hifadhi za misitu nane zenye ukubwa wa hekta 483,508.4, hifadhi za misitu ya mazingira asilia ikiwamo ya Itulu Hills yenye hekta 403,625.62.

Nyingine katika orodha zilizopandishwa hadhi ni Pindiro, hekta 8,965.3; Pugu -Kazinzumbwi, hekta 8,965.3; Uzigua hekta 27,654.58, Essimingori hekta 5,694; Uvinza hekta 1,7971; East Matogoro hekta 3,533 na Hasama Hills, hekta 3,815.9.

**MIZINGA NYUKI**

Katika uzalishaji wa mizinga, anasema wakala huo umefanikiwa kuzalisha mizinga 2,977 kwa ajili ya kuigawa kwa wananchi wafugaji nyuki na kuzalisha mazao ya nyuki.

Katika eneo la ushirikishwaji wa wananchi na kuwapunguzia utegemezi wa maisha hususani katika kulinda hifadhi za misitu, wakala huo umegawa miche 27,179,339 yenye thamani ya Sh.bilioni 10,472,359,100 na mizinga 1,256 yenye thamani ya Sh.milioni 144,500,000.

Pia, inatajwa mgawo wa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh.bilioni 1,634,665,717 kwa jamii zinazozunguka misitu.

Hiyo inaendana na mafunzo mbalimbali yanayotolewa kwa wananchi, ikiwamo vikundi 339 vya wafuga nyuki vyenye watu 5,463, wafanyabiashara 4,965 wa mazao ya misitu na nyuki na kamati za maliasili za vijiji 204.

Mengine katika orodha hiyo ni mafunzo ya moto na uhifadhi yaliyotolewa kupitia mikutano katika vijiji 903 programu za TV 37, redio 85 na makala za kuchapishwa 8,987.

Kuhusu utatuzi wa migogoro, anasema kupitia utekelezaji wa maazimio ya Kamati ya Migogoro ya Mipaka ya Mawaziri wa Kisekta, TFS imetatua migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na wananchi katika vijiji 423 kati ya 438 sawa na asilimia 97.

Anaeleza kwamba migogoro hiyo imetatuliwa katika hifadhi 39 kati ya 50 sawa na asilimia 78, huku vigingi 1,037 na mabango 103 yamewekwa katika mipaka ya maeneo hayo.

Prof. Silayo anafafanua kwamba, wakala wake unatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia mpango mkakati unaoandaliwa kwa kipindi cha miaka mitano, unaotoa dira ya usimamizi wa misitu ya serikali kuu nchini.

Kwa mujibu wa wakala huo, misitu ni rasilimali zote zitokanazo na misitu ikiwamo mazao ya mbao, matunda, mbegu, dawa, huduma za kiikolojia kama vile maji, nishati, makazi, na bioanuai na utalii.

Miongoni mwa aina za misitu inayotajwa na TFS ni misitu ya milima, Miombo, Misitu ya Ukanda wa Chini, Misitu ya Ukanda wa Pwani, Ndarambwe, Misitu ya Mikoko na mashamba ya miti.

AFYA

# Rais Samia anavyodumu 'kumimina' pesa kwenye afya zao mama na mtoto

**Na Pilly Kigome**

TANGU juzi kunaendelea kushuhudiwa shamrashamra za kumpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kufikisha miaka mitatu ya uongozi wa nchi.

Huyo ni mama, ambaye kuwapo kwake na matendo yake katika nafasi hiyo, kunaakisi mengi katika maendeleo yake.

Eneo mojawapo ambalo sasa linabeba tafsiri ya maendeleo, ni afya kukiwapo yasiyopimika na ya kufurahisha, yakitia matumaini ya kukomboa Mtanzania.

Hapo katika nafasi ya kipekee kwenye eneo chanda na pete na mwanamama; mahsusi katika uangalizi wa afya ya uzazi, mama na mtoto, kuna mengi sasa yanayoonekana.

Katika safari miaka mitatu ya serikali, 2021 hadi 2024 kunaonekana uwekezaji katika kada hiyo ya mama na mtoto.

Ndani ya Serikali ya Awamu ya Sita, Mama akiwa kashika usukani, kukaanzishwa wodi maalum kwa ajili ya huduma za watoto wachanga wagonjwa (Neonatal Care Units-NCU).

Taarifa ya Wizara ya Afya, inafafanua kwamba jumla ya hospitali 189 zimekuwapo hadi Desemba mwaka jana, ikilinganishwa na hospitali 165 za mwaka mmoja kabla, wakati nyuma mwaka 2018 zilikuwapo 14 pekee.

Lingine linatajwa ni kuimarishwa upatikanaji bidhaa za afya ya uzazi, mama na mtoto katika vituo vinavyomilikiwa na serikali, zikiongezeka kutoka asilimia 82.5 mwaka 2021 hadi asilimia 88.2 mwishoni mwa mwaka jana.

Pia kuna eneo linalotajwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kwamba Machi 18 mwaka huu, akisema juhudi kubwa zilizofanywa katika miaka mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ni pamoja na kuanzisha mfumo unaoitwa M-Mama, ambao ni wa kielektroniki.

Ni mfumo unaoratibu rufani kwa kusafirisha kinamama wajawazito na watoto wachanga waohitaji wa huduma za dharura, kutoka ngazi ya jamii hadi kwenye vituo vya kutoa huduma za afya au ngazi ya juu.

Waziri Ummy anasema, mfumo huo mwaka 2022 hadi 2023, umeendelea kufanya kazi katika mikoa yote 31 Tanzania Bara na Visiwani.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, wakisalimia watoto katika ziara zao za kikazi. **PICHA: MTANDAO**

### SARATANI KIZAZI

Kuimarisha huduma za saratani ya mlango wa kizazi, Waziri Ummy anasema jumla ya mashine 140 za uchunguzi wa saratani zenye thamani ya shilingi bilioni 1.1, zimenunuliwa na kusambazwa kwenye vituo 140 vya kutoa huduma za afya, katika jumla ya halmashauri 104 ndani ya mikoa 26 nchini.

Hiyo inaendana na wahitaji 46,941 wamenufaika katika huduma za dharura za rufani, kati yao kinamama wako 38,560 sawa na asilimia 82 na watoto wachanga walikuwa 8,273, sawa na asilimia 17. Pia, mama pamoja na mtoto kwa pamoja walikuwa 108, ambao ni asilimia moja.

Inatajwa na Wizara ya Afya, kwamba uwekezaji huo hado sasa una matokeo makubwa katika kuimarisha ubora wa huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto kupitia viashiria vikuu vinavyotumika kupima mwenendo wa ubora wa huduma kwa nchi wanachama wa Shirika la Afya Duniani(WHO), Tanzania ikisifika nafasi nzuri kwa viwango na tija katika huduma afya ya uzazi.

### KUJIFUNGUA HOSPITALI

Wizara ya Afya katika taarifa yake, inafafanua ongezeko la wajawazito katika vituo vya kutoa huduma za afya nchini, kutoka asilimia 63 mwaka 2021 na kufikia asilimia 85 mwaka jana, lengo la nchi likiwa kufika asilimia 95 ya wanaojifungua kwenye vituo vya kutoa huduma za afya ifikapo 2030.

Waziri Ummy anafafanua kwamba, Wizara ya Afya inapunguza vifo vya wanawake wajawazito kwa asilimia 80; pia kupunguza vifo vya wajawazito vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 wa sasa. Vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kutoka vifo 67 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 43 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2022.

Hiyo inatajwa kuendana na vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka vifo 43 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2016, hadi kufikia vifo 33 kwa kila vizazi hai 1,000 wa leo.

Mjini Mbeya, serikali ya sasa inaendelea kukamilisha ujenzi wa jengo la kuhudumia la mama na mtoto katika Hospitali ya Meta, inayotumika na imegharimu shilingi bilioni 13.2.

Pia, kuna ujenzi wa majengo ya huduma za Mama na Mtoto kwenye hospitali za rufani a za mikoa; ni Sekou Toure (Mwanza), Geita, Simiyu, Mawenzi (Moshi ), Njombe na Songwe, zikishagharimu shilingi bilioni 71.1.

Pia inatajwa kuimarika huduma za upasuaji wajawazito kwa kuongeza vituo vyenye uwezo wa kutoa huduma za upasuaji wa dharura kumtoa mtoto tumboni (CEMoNC) kutoka vituo 340 mwaka 2021 hadi 523 mwaka jana.

## SAMIA AONYESHA 'UMAMA' ALIPOTOA DARASA MTOTO ALIVYO NA ANAVYOLELEWA

Inatoka Uk. 11

Aidha, Dk. Samia anawataka wazazi na walezi kutenga muda wa kulea watoto wao kuacha visingizio kuwa wana shughuli nyingi na kusababisha watoto wajilee au kulelewa na watu wengine.

"Tunahitaji kutafakari na kuchukua hatua, ukosefu wa malezi ya wazazi na walezi kwa watoto wao ni miongoni mwa baadhi ya vikwazo katika malezi ya watoto wetu, hivyo tuchukue hatua," anasema. Aidha, anafafanua serikali imeandaa na inatekeleza Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ya miaka mitano na kwamba ingawa ni nchi kubwa, lakini kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo; programu hiyo inatekelezwa kote nchini.

Lingine analofafanua Rais katika kuonyesha utashi wa utekelezaji wa programu hiyo, kwa mwaka ujao wa fedha 2024/25, serikali imeelekeza mikoa na halmashauri zote kutenga bajeti za kutekeleza afua za malezi na makuzi ya watoto.

"Katika kipindi cha miaka miwili ya utekelezaji wa programu hii, tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa, mtaalamu kutoka Tanzania atawasilisha mada kuhusu uratibu na utekelezaji wa programu hiyo, hivyo atafafanua kwa kina kuhusu utekelezaji huo," anasema.

### HALI ILIVYO DUNIANI

Inaelezwa kuwa, kuna jumla ya watoto milioni 250 duniani, wengi kutoka nchi zenye kipato cha kati, wako katika hatari ya kutofikia ukuaji kamili, chanzo ikiwa ni ukosefu wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto. Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) nchini, Dk. Charles Moses, anafafanua kuwa shirika lake na wadau wengine wa afya, wataendelea kuipa kipaumbele ajenda ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kwa kuwa ni miongoni mwa wanayoyapa uzito.

"Dunia kwa sasa inakadiriwa kuwa na watoto milioni 250, wengi wao wakiwa wanatoka katika nchi za kipato cha kati, ambao wana uwezekano wa kuwa katika hatari ya kutofikia ukuaji kamili," anasema Dk. Moses.

MAZINGIRA

## WIKI YA MAJI DUNIANI...

# Ubia na taasisi binafsi unavyofanikisha mapinduzi ya Muungano kupatikana maji

**Na Frank Monyo**

KESHO ni kilele cha Wiki ya Maji inayoendelea. Msingi wake, maji yanatafsiriwa sio tu rasilimali, bali chanzo cha uhai. Mwasisi wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, alipenda sana kutumia msamiati huo. Ukweli upo, kwamba hata usalama wa jamii na uchumi, unategemea kwa kiasi kikubwa uwapo wa maji.

Kwa kutambua hilo, Umoja wa Mataifa ulitenga siku ya kesho, yaani Machi 22 kuwa Siku ya Maji Duniani. Hiyo, inatukumbusha namna mchango mkubwa unaotolewa na rasilimali umaji katika kuimarisha maisha na kuwezesha maendeleo.

Tangu kuundwa kwake mwaka 1993, Siku ya Maji Duniani imeendelea kutilia mkazo uwapo wake, pia usimamizi bora wa rasilimali hiyo muhimu. Mwaka huu, kaulimbiu kimataifa ni 'Maji kwa Ajili ya Amani'. Tanzania inaungana na wadau wengine duniani kuhakikisha kuwapo usalama wa maji.

Tangu mwaka 1998 kabla Siku ya Maji Duniani kurasimishwa, Tanzania ilikuwa ikiadhimisha umuhimu wake kusherehekea Wiki ya Maji, iliyoainishwa na Siku ya Maji Duniani, baada ya kurasimishwa kwake.

Ni mustakabali ambao Wizara ya Maji, imekuwa ikisherehekea Wiki ya Maji katika mlolongo wa matukio kati ya Machi 16 hadi 22.

Mwaka huu kaulimbiu inaangukia 'Usalama wa Maji kwa ajili ya Amani na Utulivu, ikishabiana na ya kimataifa.

Safari ya Tanzania kutimiza azma ya usalama wa maji, ni kielelezo cha dhamira na malengo ya usimamizi endelevu wa rasilimali maji.

Ni kwa kutambua usimamizi yakinifu wa rasilimali hiyo msingi, haiwezi kubaki jukumu la serikali pekee. Wizara ya Maji inatumia mfumo wa usimamizi wa rasilimali unaohusisha sekta, pia wadau wote kwa ujumla.

Ufahamu huo unaifanya Wizara ya Maji kufanya usimamizi jumuishi wa rasilimali za maji, ikiendana na usimamizi huo katika vidakio vya maji.

Malengo hayo ya kimkakati yanasisitizwa zaidi na miongozo kama vile: Sera ya Maji ya Mwaka 2002; Sera ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya Mwaka 2009, iliyofanyiwa maboresho mwaka 2022.

Mikakati hiyo inaweka misingi ya kuanzishwa kwa mifumo ya muhimu katika usimamizi wa rasilimali za maji kama vile Bodi ya Taifa ya Maji, bodi za mabonde na taasisi za watumiaji maji.



Mafundi wa maji wakiwa kazini, Mbalizi, Mbeya. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Vilevile kukaanzishwa Jukwaa la Wadau wa Sekta Mtambuka, katika usimamizi na maendeleo ya rasilimali za maji. Lengo kuu hapo linatajwa ni kuimarisha ushirika na mchango wa wadau wa maji katika hatua zote muhimu.

Uanzishwaji na utendaji kazi wa mihimili hiyo ya msingi katika usimamizi wa rasilimali za maji, unahitaji ushirikiano na wadau kutoka sekta mbalimbali.

Ndani ya mtazamo huo, Wizara ya Maji imeendeleza ushirikiano na wadau mbalimbali, katika kutengeneza majukwaa ya wadau, pia kutekeleza mipango mikakati ya usimamizi wa rasilimali za maji.

### TAASISI WADAU

Hapo ndipo kunajitokeza Taasisi ya Global Water Partnership, iliyo katika makubaliano ya ushirikiano (memorandum of understanding) na Wizara ya Maji Tanzania Bara, pia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), hususan vipengele kama vile programu za maendeleo, ukusanyaji rasilimali, kukuza uwezo na uendeshaji wa matukio ya kitaifa na kimataifa.

Kupitia makubaliano hayo, GWPTZ inashirikiana na sekta za maji Tanzania Bara na Visiwani, kutekeleza mipango kama uendeshaji jukwaa la wadau wa sekta mtambuka (NMSF) kupitia kinachoitwa kitaalamu 'Global Water Leadership Program'.

Kimsingi, ni programu inayosimamia mipango ya maji duniani, ikifadhiliwa na Asasi ya FCDO; Taasisi ya Jumuiya ya Madola inayohudumia matatizo ya kijamii kimataifa.

Programu hiyo ya maji hadi sasa nchini ni zaidi ya mwaka mmoja katika kuimarisha makundi matatu ya jukwaa la wadau wa sekta mtambuka (NMSF).

Makundi hayo matatu yalifanya kazi kwa pamoja katika kuainisha vizuizi vya utekelezaji wa usimamizi wa rasilimali maji ulio thabiti, dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Lengo kuu la mpango huo, linatajwa lilikuwa kuunda mipango mikakati, pamoja na mipango ya uwezeshaji kifedha, kutatua changamoto zilizobainika.

Eneo lingine linatajwa ni kuimarisha vikosi kazi vya jukwaa la wadau wa sekta mtambuka ambako ni chachu katika kutia nguvu mihimili ya usimamizi wa maji nchini, hata ukachangia usimamizi wa rasilimali za maji.

### KUTOKA WIZARANI

Dk. George Lugomela, Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji katika Wizara ya Maji, anayewasihi wadau wengine kuunga mkono jitihada hizo, pia anafafanua:

"Mchango wa kifedha na kitaalamu kutoka kwa taasisi ya Global Water Partnership katika kuimarisha utendaji wa vikosi kazi vya jukwaa umeleta mwamko katika sekta.

"Umehimiza pia, umuhimu wa ushirikiano katika kutatua changamoto za usimamizi wa rasilimali za maji na ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi katika sekta ya maji."

Inatajwa, mchango wa asasi ya Global EWater Partnership Tanzania (GWPTZ), katika kufanya mipango ya kisera na kimikakati, umezaa matunda bayana kupitia miradi inayogusa jamii moja kwa moja.

Hapo Dk. Lugomela, ana mfano hai wa uchimbaji wa birika (bore hole) linalotumia umeme wa nguvu ya jua, pia kujengwa josho la kunyweshea mifugo eneo la Ruvu Darajani, ikilinda vyanzo vya maji.

Orodha ya jitihada anajumuisha, kujengwa jengo la kisasa litakalotumika kama ofisi na jumuiya ya watumiaji wa maji wa Mvuha katika Bonde la Wami Ruvu. Jitihada hizo zilifanyika katika Uvuli wa Mradi wa 'Intra African Caribbean and Pacific - Global Climate' Change Alliance, programu uliofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU).

### KINACHOFANYIKA SMZ

Taasisi ya Global Water Partnership Tanzania, imekuwa ikitoa ushirikiano kwa serikali ya Zanzibar kupitia Wizara ya Maji, Nishati na Madini.

Hiyo hufanyika katika malengo kadhaa, ikiwamo kuchangia kitaalamu tafiti za uchunguzi wa maji ardhini, kurejea sera za maji, kuwezesha mkutano wa maji Zanzibar wa maji kila mwaka.

Mkutano wa maji umekuwa na mchango mkubwa katika kuwakutanisha wadau kama vile watunga sera, wadau wa maendeleo, watafiti, wanasayansi, sekta binafsi pamoja na wadau mbalimbali wa maji.

Asasai Global Water Partnership Tanzania pia imekuwa mstari wa mbele kutekelezai mradi uitwao 'Africa Water Investment Program' (AIP) (Programu ya Uwekezaji Maji Afrika), chini ya ushirika wa Global Water Partnership.

Zanzibar kwa sasa imekuwa nchi ya kwanza kutekeleza chini ya Rais Dk. Ali Hassan Mwinyi, kukiwekezwa kiwango Dola za Marekani 665 millioni mnamo March 2022.

Hadi sasa Global Water Partneship Tanzania inashirikiana na Wizara ya Maji SMZ kuratibu uwekezaji Tanzania.



Mradi wa maji wenye ufanisi ulioko Pemba.



# JKT kudhibiti wavamizi bonde la Makutupora

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BODI ya Maji Bonde la Wami Ruvu imeingia makubaliano na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kikosi cha 834 Makutupora kulinda Bonde la Hifadhi ya Maji Makutupora kudhibiti watu kuvamia na kufanya shughuli za kibinadamu.

Eneo hilo lenye ukubwa wa kilimeta za mraba 348.26 ni chanzo kikubwa cha maji kinachotegemewa kuhudumia Jiji la Dodoma kwa asilimia 90.

Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu, Mhandisi Elibarik Mmassy, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hatua zilizochukuliwa na serikali kulinda hifadhi hiyo ya maji.

Alisema bonde hilo liligunduliwa mwaka 1954 kuwa ni hifadhi ya maji, hivyo serikali hadi sasa imewekeza kiasi cha Shilingi trilioni moja kwenye miundombinu mbalimbali ikiwamo umeme, barabara na ujenzi wa matangi makubwa ya maji.

"Ili bodi hili kuwa salama sisi Bodi ya Maji Bonde la Wami Ruvu kupitia Wizara ya Maji na Serikali tumeona chanzo hiki kinapaswa kulinda kwani ndiyo sehemu pekee inayotegemea na Jiji la Dodoma kwa kuwa mkoa huu hauna mito wala ziwa."

"Tumeamua kuingia makubaliano na JKT, kuwatumia wao kulinda bonde hili la hifadhi maji Makutupora kwa kutoa pikipiki nne ambazo zinatumika kufanya msako, lakini pia droni ambayo itatumika kupiga picha na kutoa taarifa kama kuna uvamizi wowote unaendelea ili hatua kuchukuliwa," alisema.

Alisema hali hiyo imefikia baada ya kuwapo kwa uvamizi mkubwa wa watu kuingia katika hifadhi hiyo ya maji na kufanya shughuli za binadamu hali inayohatarisha kuharibu chanzo hicho.

"Watu hivi sasa wanavamia na kufanya shughuli za kilimo, kuchunga mifugo, uwindaji, kuchoma moto na kujenga makazi, hivyo kupitia picha za droni hii tunayoikabidhi kwa JKT itasaidia kutoa taarifa na shughuli hizo kusimamishwa mara moja," alisema.

Alisema katika mwaka wa fedha 2024/25, bodi hiyo imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 1.2 kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwamo kuongeza mifumo ya kiulinzi ya eneo hilo.

"Pia fedha hizo kiasi kitatumika kutoa mizinga kwa ajili ya ufugaji nyuki kwa wakazi wa eneo linalozunguka hifadhi hii ya maji ili wawe na shughuli ya kuwaingizia kipato, lakini pia tutajenga maeneo kwa ajili ya kunyweshea mifugo ili kuondoa tatizo la wafugaji kuharibu miundombinu ya mabomba ili wapate maji ya mifugo yao," alisisitiza.

Kefa Malima, mkazi eneo hilo, alishukuru serikali kwa kuwapatia mizinga na kujenga maeneo ya kunyweshea mifugo hali ambayo itasaidia bonde la hifadhi ya maji Makupora kulindwa.

## Bil. 1.6 /- kukabili mabadiliko tabianchi

**Na Peter Mkwavila,** MPWAPWA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, amesema Shilingi bilioni 1.6 zimetengwa kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi nchini.

Alitoa kauli hiyo jana kwenye hafla ya kugawa cherehani kwa vikundi vitatu vya ushonaji vya Kijiji cha Kiegea, Mbugani na Kazania wilayani Mpwapwa iliyoambatana na uzinduzi wa kisima cha maji kwenye vijiji hivyo.

Jafo, alisema fedha hizo za mradi wa kuhimili mabadiliko hayo kwa kutumia mifumo ikolojia vijijini (EBARR) zinatumika kutekeleza shughuli mbalimbali na wilaya tano zimeanza kunufaika.

Alitaja miradi hiyo inayotekelezwa kupitia fedha hizo kuwa ni kujenga birika za kunyweshea mifugo, vitalu nyumba, nyumba za nyuki, ununuzi wa ng'ombe, mbuzi, vifaranga vya kuku, boti za kisasa za uvuvi zilizonunuliwa Kaskazini A, visima vya maji na shamba darasa.

Alisema wilaya zinazotekeleza EBARR ni Kaskazini 'A' visiwani Zanzibar, Mvomero mkoani Morogoro, Mpwapwa (Dodoma), Simanjiro (Manyara) na Kishapu (Shinyanga).

Jafo, alisema EBARR inasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa lengo la kuinua uchumi kwa wananchi kujipatia kipato kwa vikundi kwa ajili ya shughuli zao.

Diwani wa Kata ya Ngh'ambi, Richard Matonya, alisema kabla ya mradi huo wa kisima utawaondolea kero wananchi ya kwenda kuchota maji umbali wa zaidi ya kilometa 10.

Mratibu wa EBARR Kitaifa, Dk. Makuru Nyarobi, alisema lengo la miradi hiyo ni kuwasaidia wananchi katika shughuli zao hasa uchumi.



Kamishna wa Walipakodi Wakubwa wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Michael Muhoja (kulia), akikabidhi Tuzo ya Mlipakodi Mkubwa kwa kuhamasisha utalii nchini kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Hoteli ya Serena, Ashis Sharma, katika hafla ya kukabidhi tuzo kwa walipakodi kwa mwaka 2023, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TNMC yataja anguko mitihani ya uuguzi, ukunga

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BARAZA la Uuguzi na Ukunga (TNMC) limesema anguko la wanafunzi wanaofanya mtihani wa umahiri linatokana na kukosa stadi za mafunzo ya vitendo kwenye maeneo ya kutolea huduma.

Hivi karibuni wanafunzi 1,228 walirudia mtihani, kati ya hao, waliofaulu ni 426 sawa na asilimia 34 huku wengine 802 hawakufanya vizuri na kutakiwa kurudia tena mtihani huo.

Msajili wa Baraza hilo, Agness Mtawa alitoa kauli hiyo jana kwenye kumbukizi ya Miaka 71 ya utoaji huduma iliyoambatana na kutoa misaada katika Kituo cha Afya Makole jijini hapa.

Agness alifafanua kuwa wanafunzi 802 waliofeli mtihani huo, wameshauriwa kuendelea kwenda maeneo ya kutolea huduma ili kupata ujuzi ikiwamo misingi ya uuguzi, kuwasaidia wagonjwa waliofanyiwa upasuaji na walio kwenye tiba.

"Kwenye mitihani yetu hakuna kikomo ufanyaji mitihani tunasema hadi pale utakapofaulu mtihani basi tutakusajili na tunawahimiza pia wanapoanguka waangalie maeneo ambayo hawajafanya vizuri ili kuendelea kujikumbusha kwa kufanya mafunzo kwa vitendo," alisema na kuongeza kuwa:

"Pia jukumu letu ni kuhakikisha hata wale wanaopewa leseni wana viwango na weledi wa kutosha na mtihani wa baraza unalenga umahiri wa maeneo ya kutolea huduma kwa hiyo inapotokea anguko kwa wanafunzi tunafikiri hawakupata stadi za sehemu za kutolea huduma."

Aliwaasa wanaohitaji kusajiliwa na baraza hilo kwenda sehemu za kutolea huduma kupata stadi na weledi kutosha na watakapofanya mitihani wafaulu ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Kabla ya kufanya mtihani nenda maeneo ya kutolea huduma, tunataka tuwe na wauguzi na wakunga wenye weledi ambao watatoa huduma bora kwa wananchi," alisema.

Muuguzi Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Dk. Situ Muhunzi, alisema wamekuwa wakipokea wauguzi na wakunga wanaojitambua kutokana na misingi imara ya baraza hilo.

"Wananchi wengi wa Jiji la Dodoma wanahudumiwa hapa na malengo ni kuhudumia kinamama 71 kwa mwezi, lakini tunahudumia 600 hadi 700, wauguzi hawa hawa wanatoa huduma ya kliniki kwa kinamama na watoto 150 kwa siku ni kwa sababu ya weledi wao wananchi wanawakimbilia," alisema..



# Wakulima wa mahindi walia ukosefu wa soko

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKULIMA wa mahindi mkoani Njombe wamesema wamekosa soko la kuuza mazao yao, hali iliyosababisha walanguzi kuanza kununua kwa bei ndogo ambayo inawaumiza.

Waliyasema hayo wakati wa kikao cha wadau wa kilimo kilichoandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) chini ya mradi unaolenga kusaidia taasisi za wakulima kwa nchi za Afrika, Caribean na Pacific (FO4ACP) kilichofanyika mkoani hapa.

Walisema baadhi ya wakulima hawana maghala ya kuhifadhi mahindi, hivyo soko la uhakika linapokosekana wanalazimika kuuza kwa bei ndogo wakihofia kuharibika.

Walibainisha kwamba wapo wanunuzi ambao wakati mwingine wanajitokeza lakini wananunua kiasi kidogo cha mahindi, hivyo kusababisha wakulima kubakia na mahindi mengi na wasijue sehemu ya kuuza.

Mmoja ya wakulima hao wa mahindi ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Vikundi Amani (UVIA) kilichopo wilayani Ludewa, Oddo Mlowe alisema Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) Kanda ya Makambako walifika kwenye Kijiji cha Amani na kununua mahindi tani 1,800 na kiasi kilichobaki ni zaidi ya tani 3,000.

"Tunaomba taasisi za fedha kama inawezekana ingetupa mtaji wa kuwa na stakabadhi ghalani tungeweza kupata mazao kwa wingi zaidi na kunusuru wananchi wetu kuuza mahindi kwa bei nafuu," alisema Mlowe.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Njombe (NJORECU), Stephano Luoga, aliwaomba NFRA kutoa kipaumbele kwa vyama vya ushirika kwa kuwa mwaka jana hali ya vyama hivyo haikuwa nzuri kutokana na kushindwa kuuza mahindi.

Aidha, alisema madhumuni ya kuanzisha ushirika ni pamoja na kupata soko, hivyo mwaka jana vyama havikupewa kipaumbele hali iliyosababisha kushindwa kuuza mazao.

Ofisa Ubora kutoka NFRA Makambako, Josephat Ringo, alisema wanatoa mikataba na kipaumbele huwa ni kwa vyama vya ushirika, lakini changamoto inayojitokeza ni kuwa uzalishaji unatofautiana kulingana na majira.

Hata hivyo alisema kuna muda wanaingia mikataba na vyama lakini wanashindwa kupeleka hata tani moja ya mahindi mpaka msimu unaisha.

"Kwa maana ya kwamba kama uzalishaji ni mdogo na wafanyabiashara wapo wa kutosha msimu huo upatikanaji wa mahindi utakuwa ni mdogo," alisema.

Awali akifungua kikao hicho Katibu Mtendaji wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC), Florian Haule, alivitaka vyama vya ushirika kujiendesha kibiashara na kuacha kufanya shughuli zao kwa mazoea.

Alisema ili vyama vijiendeshe kibiashara lazima taasisi za fedha zishirikishwe na waweze kutambua kuwa vyama hivyo vina mahitaji ya mikopo na kama kuna changamoto ya kusababisha kushindwa kukopesheka waweze kuelezwa.

Alisema: "Kwa sasa hivi dunia tunakokwenda mikutano ya kibiashara ndiyo jukwaa pekee linalowakutanisha kati ya wale wanaotoa huduma fulani na wasambazaji wa hiyo huduma kwa kukaa na kujadili na kukubaliana tunaweza kuingia kwenye biashara."



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), wakipanga mawe, ili kuanza ujenzi wa tangi la kuhifadhia maji katika eneo la Forest Mpya jijini Mbeya juzi, ambalo ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Chanzo cha Mto Kiwira. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Bil. 42/- kuziunganisha H'shauri za Rungwe, Busokelo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 42 kwa ajili ya kujenga Barabara ya Katumba-Mbambo-Tukuyu inayounganisha halmashauri za Rungwe na Busokelo mkoani Mbeya kwa kiwango cha lami.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADs) Mkoa wa Mbeya, Masige Matali, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya barabara mkoani hapa katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema barabara hiyo imeshaanza kujengwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha na kwamba imegawanywa katika vipande vitatu ambavyo viwili tayari vimeanza na kimoja pekee ndicho kimebakia.

Alisema vipande ambavyo vinaendelea kujengwa ni Bujesi-Mbambo (km10) na kipande cha Tukuyu-Mbambo (km7).

"Vipande vyote hivi vinajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 21.3 na kipande kilichobakia kitaanza kujengwa hivi karibuni na kina urefu wa kilomita 35.3," alisema Matali.

Alisema mradi huo ukikamilika utawarahisishia wananchi wa Busokelo kusafiri na kusafirisha mazao yao kutoka mashambani kwenda sokoni pamoja na kusafirisha pembejeo za kilimo.

Hivyo hivi karibuni baadhi ya wananchi wa Busokelo walisema barabara hiyo ikikamilika itawasaidia kupunguza gharama za usafiri wakidai kuwa kwa sasa wanatumia gharama kubwa.

Lusekelo Mwaijande alisema kwa sasa nauli ya kutoka Lwangwa yalipo makao makuu ya Busokelo ni Sh. 6,000 mpaka Sh.7,000 lakini barabara ikikamilika nauli itashuka na haitazidi Sh. 4,000 na kwamba hata muda wa kusafiri utapungua.

Alisema kwa sasa wanatumia saa mbili na nusu mpaka tatu lakini ujenzi wa barabara hiyo ukikamilika kuna uwezekano muda ukapungua na kuwa chini ya saa moja pekee.

"Wakati mwingine mvua ikinyesha unakuta magema yameshuka na kufunga barabara lakini ikijengwa ya lami haya mambo yatakwisha, lakini kipindi kama hiki cha mvua nyingi barabara yetu huwa inateleza sana kwa hiyo magari yanakwenda taratibu," alisema Mwaijande.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alipofanya ziara wilayani humo aliagiza ujenzi wa barabara hiyo ukamilike mapema na kwa kiwango kinachotakiwa ili kuifungua Halmashauri ya Busokelo.

## Miradi miwili kumaliza tatizo ukosefu wa maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya WSSA), imetenga Sh. bilioni 10 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi miwili ya maji inayotarajiwa kumaliza tatizo la upatikanaji wa maji katika Jiji la Mbeya na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Kaimu Mkurugenzi wa Mbeya-WSSA, Barnabas Konga, aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya waandisi wa habari ya kutembelea baadhi ya vyanzo vya maji vinavyosimamiwa na mamlaka hiyo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Maji Duniani.

Konga aliitaja miradi inayotekelezwa kuwa ni Mradi wa Chanzo cha Maji cha Mwasekwa ambacho kinatarajiwa kuhudumia zaidi ya wananchi 40,000 wa kata tatu za jiji hilo na Mradi wa Maji wa Ilunga ambao unatarajiwa kuhudumia zaidi ya wananchi 100,000 wa Mji wa Mbalizi na baadhi ya maeneo ya Jiji la Mbeya.

Konga alisema mradi wa Mwasekwa unagharimu Sh. bilioni 5.2 na wa Ilunga unagharimu Sh. bilioni 4.8 na kwamba miradi hiyo ni kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la upungufu wa maji katika kipindi cha mwaka mmoja.

"Mahitaji ya maji katika Jiji la Mbeya na Mji wa Mbalizi ni lita za ujazo milioni 90 lakini kwa sasa uzalishaji ni lita za ujazo milioni 66.5, kwa hiyo ili kufikia lengo ndiyo maana tunatekeleza miradi hiyo ya muda mfupi wakati tukisubiri mradi wa chanzo cha Mto Kiwira," alisema Konga.

Alisema tatizo linaloikabili mamlaka hiyo na kusababisha kuwa na upungufu wa maji katika baadhi ya maeneo ni upotevu wa maji unaotokana na kupasuka kwa mabomba yaliyochakaa, uunganishaji wa maji holela unaofanywa na baadhi ya wananchi pamoja na ujenzi wa barabara.

Meneja wa Uendelezaji wa Miundombinu wa Mbeya-WSSA, Deogratius Leonidas ambaye anasimamia utekelezaji wa mradi wa Mwasekwa alisema mradi huo umekamilika kwa zaidi ya asilimia 70 na kwamba wananchi tayari wameanza kupata huduma.

Alisema wameshakamilisha ujenzi wa chanzo pamoja na eneo la kusafishia maji na kwamba kilichobakia kwa sasa ni ujenzi wa tangi la kuhifadhia maji ambalo alisema wanatarajia kulikamilisha kabla ya Juni mwaka huu.

Alisema kwa sasa wanazalisha maji kutoka kwenye chanzo na kwenda moja kwa moja kwa wananchi, jambo ambalo alisema limesaidia kupunguza shida kwa wananchi wa maeneo yanayolengwa.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi wa maeneo husika ili waunganishiwe huduma hiyo na kwamba mpaka sasa wana maombi zaidi ya 100 ya wananchi wanaotaka kuunganishiwa.

Naye Meneja wa Mradi wa Ilunga, Uswege Mwaipopo, alisema mradi huo umekamilika kwa asilimia 98 na kwamba kazi zilizobakia kwa sasa ni umaliziaji wa baadhi ya maeneo machache yaliyobaki.

Alisema kwa sasa eneo kubwa wanaloendelea na ujenzi ni la kusafishia na kutibia maji na kwamba maji tayari yameshafika kwa wananchi kutokana na mradi huo kusafirisha maji kwa njia ya mseleleko.

Alisema mradi huo kwa sasa tayari umeshaanza kuwahudumia wananchi wa Kata ya Iwambi jijini Mbeya na vijiji vya Idugumbi na Itimba vilivyoko katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.



# Serikali Z'bar yaanza mkakati kutokomeza ufaulu daraja sifuri

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuweka mazingira mazuri na wezeshi ya kujisomea na kufundishia, ili kuzidisha ufaulu wa daraja la kwanza na kuhakikisha inatokomeza ufaulu wa daraja sifuri.

Hayo yalisemwa jana na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla wakati wa utoaji futari kwa wanafunzi wanaoishi dahalia (bweni) pamoja na wananchi wa Kiwani Kisiwani Pemba.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa elimu na hali halisi ya maisha ya dahalia wameona ipo haja ya kula futari pamoja na wanafunzi wanaoishi dahalia kwa kuwapatia futari ambayo itawasaidia na kazi yao ni kusoma kwa faida yao na taifa kwa ujumla.

Hemed alisema kuwa mkakati wa serikali ni kuhakikisha wanafunzi wote wa kidato cha nne na sita wanapata alama ya ufaulu daraja la kwanza jambo ambalo linahitaji ushirikiano baina ya walimu, wanafunzi na wazazi ambao utawawezesha kwa urahisi kwa mwanafunzi kupata ufadhili wa masomo ndani na nje ya nchi.

Aidha aliwataka wanafunzi kuongeza bidii katika masomo yao ili kupata viongozi waliobora na wenye kuelimika ambao watakuja kulitetea taifa kwa kuendeleza miradi ya maendeleo.

Hata hivyo aliitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuhakikisha wanapeleka walimu wa kutosha shuleni ili kupata matokeo mazuri kwa wanafunzi hasa wa kidato cha nne na cha sita.

Alisema serikali itahakikisha kila mwaka inaongeza Bajeti ya Wizara ya Elimu hasa katika kitengo cha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kutoa fursa kwa wanafunzi watakaofanikiwa kujiunga na vyuo vikuu kusoma pasipo na changamoto ya ada.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Mohamed Mussa alimpongeza Makamu wa Pili kwa kuendelea kuwasaidia wanafunzi wanaoishi katika dahalia kwa kuwapatia futari jambo ambalo linatoa ahueni ya maisha kwa wanafunzi hao.

Waziri Lela alisema walimu na wanafuzi ni vyema kuzithamini jitihada zinazofanywa na viongozi wakuu wa nchi kwa kuweka mkakati wa kutokomeza sifuri na kupata ufaulu wa daraja la kwanza kwa wanafunzi wote wa kidato cha nne na kidato cha sita.

Wanafunzi wa shule hiyo wameahidi kusoma kwa bidii na kupata matokeo mazuri katika mitihani yao kwa faida yao wenyewe na taifa kwa ujumla.

## Sheria ya kuajiri maofisa ustawi jamii kila ofisi yaiva

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Anna Paul amesema sheria rasmi inayoonesha umuhimu wa maofisa ustawi wa jamii kuajiriwa katika kila ofisi inakaribia kukamilika.

Alisema hayo jana katika hafla ya maadhimisho ya Siku ya Ustawi Duniani ambayo iliyofanyika Hospitali ya Rufani Mnazi Mmoja Zanzibar.

Alisema endapo sheria hiyo ikikamilika kila ofisi italazimika kumwajiri ofisa ustawi kwa ajili ya kuangalia na kusimamia ustawi wa watu wote wanaoingia na kupata huduma pamoja na waajiriwa.

Aidha aliwataka maofisa ustawi kutovunjika moyo katika kufanya kazi zao na badala yake waongeze bidii ili kutoa huduma bora kwa jamii.

"Kazi za kuihudumia jamii ni ngumu na katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii na afya kila moja kuna changamoto zake katika utoaji wa huduma, hivyo amesema ni lazima kufuata misingi imara ya kazi zao ili kufikia malengo," alisema.

Naye Naibu Waziri wa Afya, Hassan Ali Hassan, aliwataka maofisa ustawi kutekeleza vyema majukumu yao kwasababu malalamiko mengi ambayo yanatokea kwa watu wanaofika vituo vya afya kupata huduma yanachangiwa na kutowajibika vyema kwa maofisa ustawi wa jamii.

Aidha alisema hakuna Taifa linaloweza kuendelea bila ya kuwapo kwa maofisa ustawi wa jamii, hivyo aliwataka maofisa hao kusimamia vyema majukumu yao ili kuondoa kasoro ambazo zinajitokeza kila siku katika hospitali.



Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Sheikh Walid Alhad Omar (wa tatu kulia) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu (wa tatu kushoto) na baadhi ya viongozi mbalimbali wakipata futari iliyoandaliwa na benki hiyo jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# SMZ yaunga mkono vita kutokomeza ukatili kijinsia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Mafunzo ya Amali Zanzibar, imesema inaunga mkono jitihada za wadau katika kukemea na kuondowa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia katika maeneo mbalimbali, ikiwamo ya kijamii na vyuo vya amali.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka hiyo, Fatma Elia, aliyasema hayo juzi katika mkutano wa kupitia hati ya makubaliano ya utekelezaji wa mradi wa ushirikiano ya pamoja ya kupinga vitendo vya udhalilishaji na ukatili baina ya vyuo vya amali na Shirika la Wanawaake la Umoja wa Mataifa (Un Women).

Alisema katika maeneo hayo kumekuwa na madai ya kujitokeza kwa matukio hayo, hivyo kupitia mradi huo utakuwa chachu ya kuondosha na kuwa na taifa bora.

Aidha, alisema kuwa bodi hiyo itakuwa mstari wa mbele kufuatilia utekelezaji wa mradi huo ili kuona malengo yanafikiwa na kuishukuru UN Women kwa kupeleka mradi huo katika vyuo hivyo.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuibua hisia za watu sambamba na kuongeza uweledi kwa vijana kujikinga na vitendo hivyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Bakar Ali Silima, alisema kupitia mradi huo watahakikisha wanaimarisha mafunzo katika maeneo tofauti ili kuongeza uelewa.

Naye Mratibu wa mradi huo, Patma Khamis Rajab, alisema kuwepo kwa mradi huo katika vituo hivyo kunakwenda sambamba na utekelezaji wa sera za kuzuia unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto na kuweka mazingira salama ya vyuo hivo.

Alisema kuwa watahakikisha kupitia mradi huo watatengeneza njia za mawasiliano zinazohusu kukomesha ukatili dhidi ya wanawake na wasichana kwa vyuo vya amali na watoa huduma.

Alisemea katika utekelezaji wa mradi huo watahakikisha wanaandaa kanuni za maadili kwa wamiliki, madereva na makonda wa usafiri wa umma ili kuweka mazingira salama ya usafiri kwa kuondosha matukio hayo.

Meneja mradi wa kupinga ukatili wa kijinsia kutoka UN Women, Lusi Tesha, alisema mradi huo utawahusisha wasichana na wavulana ambapo utekelezaji wake utasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha ustawi wa vijana na taifa kwa ujumla.

Alisema lengo la mradi huo ni kupinga vitendo vya udhalilishaji hapa nchini ambapo vinaonekana kuwapo kwa kiasi kikubwa kupitia nyanja mbalimbali, ikiwamo kubakwa, kutolewa lugha chafu, kuguswa, kutelekezwa na mambo mengine.

Alisema matukio hayo hujitokeza kupitia maeneo tofauti ikiwamo katika familia, mitaani, vyombo vya usafiri, mitandaoni na maeneo mengine ambapo kwa namna moja au nyingine huleta dosari kubwa kwa mtendewa ikiwamo kuathirika kisaikolojia na kushindwa kufikia malengo yake.

Mradi huo wa ushirikiano wa pamoja kati ya UN Women na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia ufadhili wa EU utatekelezwa kwa miaka minne kwa awamu tofauti kwenye vyuo vya amali 42 vya serikali na binafsi ukitarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. bilioni 105.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**GODFREY N KHATAU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3933-0016** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **RISING STAR SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/493565/2022**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ROMAN JOACHIM ASSENGA** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki aina ya Toyo zenye namba za usajili **MC 696 ARZ** na **MC 157 ARW.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/41848/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SYILVANUS DAUDI NCHIYIKI** KAKOLWA ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 798 DGA** AINA YA **PROBOX.** TAARIFA HII IMERIPOTIWA POLISI NA KUPEWA KUMB **KAS/TR/RB/474/2024.** ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA POLISI.

---

**(Substituted Service)**
**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL FOR KAHAMA**

**AT KAHAMA**

**LAND APPLICATION No.16. 2024**

**EMMANUEL LAMECK................................APPLICANT**

**VERSUS**

**ANDREA MATHEO................................RESPONDENT**

**TO;**
**ANDREA MATHEO**

**TAKE** notice that, the above matter is coming for 22 on 03 Day of 2024 at 09:00 am Before **Hon. KAPINGA A.M.** Chairman of the Tribunal. You are hereby commanded to appear in this Tribunal in person or by Advocate or agent dully authorized when the case will be mentioned.

**TAKE FURTHER NOTICE** That, in default of your appearance on the date and time above mentioned, the suit will be heard and determined in your absence.

**GIVE** under my **HAND** and the **SEAL** of this tribunal this 08 day of 03, 2024.

CHAIRMAN

---

**(Substituted Service)**
**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL FOR KAHAMA**

**AT KAHAMA**

**LAND APPLICATION No.17. 2024**

**PASKALI FRANCIS....................................APPLICANT**

**VERSUS**

**ANDREA MATHEO...................................RESPONDENT**

**TO;**
**ANDREA MATHEO**

**TAKE** notice that, the above matter is coming for 22 on 03 Day of 2024 at 09:00 am Before **Hon. KAPINGA A.M.** Chairman of the Tribunal. You are hereby commanded to appear in this Tribunal in person or by Advocate or agent dully authorized when the case will be mentioned.

**TAKE FURTHER NOTICE** That, in default of your appearance on the date and time above mentioned, the suit will be heard and determined in your absence.

**GIVE** under my **HAND** and the **SEAL** of this tribunal this **08 day of 03, 2024.**

CHAIRMAN

---

**(Substituted Service)**
**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL FOR KAHAMA**

**AT KAHAMA**

**LAND APPLICATION No.19. 2024**

**CRESENCIA JAPHET JOHN....................APPLICANT**

**VERSUS**

**MAJUTO MATHEO.............................RESPONDENT**

**TO;**
**MAJUTO MATHEO**

**TAKE** notice that, the above matter is coming for 22 on 03 Day of 2024 at 09:00 am Before Hon. KAPINGA A.M. Chairman of the Tribunal. You are hereby commanded to appear in this Tribunal in person or by Advocate or agent dully authorized when the case will be mentioned.

**TAKE FURTHER NOTICE** That, in default of your appearance on the date and time above mentioned, the suit will be heard and determined in your absence.

GIVE under my HAND and the SEAL of this tribunal this 08 day of 03, 2024.

CHAIRMAN

---

**(Substituted Service)**
**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL FOR KAHAMA**

**AT KAHAMA**

**LAND APPLICATION No.18. 2024**

**JUMA MABULA SEGESE.......................APPLICANT**

**VERSUS**

**MAJUTO MATHEO.............................RESPONDENT**

**TO;**
**MAJUTO MATHEO**

**TAKE** notice that, the above matter is coming for 22 on 03 Day of 2024 at 09:00 am Before Hon. KAPINGA A.M. Chairman of the Tribunal. You are hereby commanded to appear in this Tribunal in person or by Advocate or agent dully authorized when the case will be mentioned.

**TAKE FURTHER NOTICE** That, in default of your appearance on the date and time above mentioned, the suit will be heard and determined in your absence.

GIVE under my HAND and the SEAL of this tribunal this 08 day of 03, 2024.

CHAIRMAN

---

**FOMU MADAI - 12**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KIGOMA**
**Kituo cha UJIJI Mkoa KIGOMA**

**Shauri la Madai/Ndoa Na. 38/2024**

**Jina la mdai: SAMSON JANUARY CHOBANKA**

**Jina la mdaiwa: EMMANUEL GODFREY KYABWASI**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(kanuni ya 62 ya Kanuni za Uendeshaji mashauri Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: EMMANUEL GODFREY KYABWASI**

Kwamba mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya kutekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe 25 Mwezi 03 Mwaka 2024 kueleza kwanini hukumu isitekelezwe dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 14 Mwezi 03 Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO UJIJI
WILAYA YA KIGOMA

---

**FORM 58**

**GENERAL CITATION**
**( Rule 75)**

**IN THE COURT DISTRICT DELEGATE OF ARUSHA DISTRICT AT ARUSHA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 4929 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the Late EDNA CHARLES MOSHI**

**And**

**In the matter of Application for probate of the Will of the late By ARNOLD CHARLES MOSHI**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate is made to the above – named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 15th day of April 2023

The will of the said deceased is deposited and open for inspection at the court

Dated at ARUSHA this 20th day of MARCH 2022

RESIDENT MAGISTRATE
PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...16/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**

**MAREHEMU: ZENA SELEMANI wa MODECO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MOSHI ALLY RASHIDI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 16 Mwezi 4 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 18 mwezi 3 mwaka 2024

..............................................
**HAKIMU**

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Marekani yaonya Israel

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imetaja kuwa watu zaidi ya milioni mbili wanaoishi Ukanda wa Gaza wanakabiliwa na kiwango cha juu cha uhaba wa chakula.

Akizungumza na Shirika la Habari la Uingereza (BBC) Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo, Antony Blinken ameonya hali hiyo ni ya kutisha na kuitaka Israel kutanguliza jukumu la utoaji misaada ya chakula kwa wanaohitaji kwa ajili ya kuwaokoa.

Hata hivyo, mashirika ya Umoja wa Mataifa yanayofanya kazi katika eneo hilo yamesema Gaza Kaskazini huenda ikakabiliwa na baa la njaa ifikapo mwezi Mei kama hakuna usitishwaji wa mapigano na kuongezeka kwa misaada.

Blinken alitoa onyo hilo wakati wa ziara yake nchini Ufilipino jana.

Marekani ni mshirika wa karibu wa Israel na mtoaji mkubwa wa misaada ya kijeshi.

Katika hatua nyingine, Marekani imeiamurua Israel kumruhusu Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuwahudumia wakimbizi wa Kipalestina (UNRWA) kuingia mji wa Gaza, baada ya Israel kumzuia kutokana na kile ilichokisema hakufuata utaratibu.

Tamko hilo la Marekani lilitolewa siku moja baada ya mkuu wa shirika hilo, Philippe Lazzarini, kulalamika kuwa Israel ilimzuia kutembelea Gaza ambayo imeharibiwa vibaya na vita.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje Marekani, Vedant Patel, alisema wana imani kuwa kiongozi hiyo ataweza kutembelea eneo la operesheni.

Aidha Patel aliongeza kuwa serikali zote nchi za kikanda zinahitaji kufanya kile kinachohitajika kuwezesha mwitikio wa kutoa misaada ya kibinadamu, sanjari na kuruhusu uingiaji huru wa wafanyakazi wa kimataifa.

Hata hivyo, hakuzungumza kama nchi yake imezungumzia hilo moja kwa moja na serikali ya Israel, ili kumruhusu kiongozi huyo kuingia Gaza.

Wizara ya Ulinzi ya Israel ilisema kuwa Lazzarini hakufuata utaratibu wakati wa kuomba kuingia Gaza.

Msemaji wa Umoja wa Mataifa, Farhan Haq, aliwaambia waandishi wa habari kwamba shirika hilo halina maelezo yoyote kwa nini kuongozi huyo amenyimwa kuingia Gaza.

Awali, Israel imeshutumu wafanyakazi 13,000 wa walihusika katika shambulio la Oktoba 7, ambalo lilichochea operesheni ya kijeshi ya Israel katika ukanda huo.

Kuunga mkono shutuma hizo, Marekani na wafadhili wengine kadhaa walisimamisha ufadhili kwa UNRWA kupisha uchunguzi, hata hivyo Waziri wa Mambo ya Nje, Antony Blinken, alitaja kazi ya shirika hilo kuwa ya thamani kubwa.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, alisisitiza kwamba bado amedhamiria kutekeleza mashambulizi ya ardhini katika eneo la Rafah, licha ya Marekani kupinga. **DW**



Askari jeshi wa Russia akitumia mchanga kuzima moto uliotokana na shambulio katika mji wa Belgorod. **PICHA: DPA**

## Waliochota bil. 102 benki kimakosa sasa wasakwa

**ADDIS ABABA** ETHIOPIA

BENKI kubwa ya kibiashara nchini Ethiopia imewataka wateja waliotoa pesa nyingi zaidi ya kiasi walizonazo katika akaunti zao kuzirudisha haraka ndani ya wiki moja.

Benki hiyo ya biashara (CBE), ilipata matatizo katika mfumo wake wa mtandao wa utunzaji fedha na kusababisha wateja waliokuwa wakitoa pesa kupata kiasi kikubwa cha fedha tofauti na kiasi walichohifadhi.

Vyombo vya habari nchini humo viliripoti kuwa zaidi ya dola milioni 40, zilitolewa au kuhamishiwa benki nyingine wakati wa hitilafu hiyo iliyodumu kwa saa kadhaa jumamosi ya wiki iliyopita.

Katika mahojiano na BBC, Rais wa CBE ambayo inamilikiwa na serikali, Abe Sano, alisema benki hiyo imefuatilia utoaji wa miamala mingi iliyofanywa wakati wa hitilafu.

Hata hivyo, Sano alisema endapo watu hao hawatarudisha itaripoti suala hilo polisi ili wakamatwe na kurudisha kinguvu.

Aliongeza kuwa benki hiyo itawachukulia hatua za kisheria wale ambao hawatakuwa wamerudisha fedha hizo ndani ya wiki hii.

"Hakuna njia ambayo hawawezi kutoroka kwa sababu sisi ni waendeshaji wa mfumo wa kidijitali na ni wateja wetu," alisema.

Aliongeza "Tunawajua. Wanaweza kufuatiliwa na wanawajibika kisheria kwa walichokifanya."

Alisema baadhi ya wateja waliotoa pesa za ziada tayari wamezirudisha katika benki hiyo.

Hata hivyo alipinga ripoti kwamba wateja walichukua dola milioni 40, akisema kiasi kilichochukuliwa kilikuwa kidogo sana lakini kitajulikana kwa usahihi baada ya ukaguzi unaoendelea.

Sano alisisitiza kuwa ukaguzi unafanywa kwa sababu baadhi ya wateja kati ya 10,000 waliofanya miamala wakati wa hitilafu walifanya miamala halali. **BBC**

## Benki Kuu ya Haiti yavamiwa

**PORT AU PRINCE,** HAITI

GHASIA zinazofanywa na magenge ya kihalifu nchini Haiti zinazidi kuiteketeza taifa hilo baada ya makundi yanayopingana kushambulia benki kuu na kusababisha vifo vya watu wanne.

Hata hivyo kulikuwa na majibizano makali kutoka kwa kundi la wahalifu waliotaka kuiteka Benki Kuu na watu waliozuia shambulio hilo na kufanya eneo hilo kuwa kiini cha mapigano.

"Kundi la wahalifu" lililenga Benki ya Jamhuri ya Haiti Jumatatu, mfanyakazi mmoja aliiambia AFP.

Uongozi wa benki hiyo ilitoa taarifa ya tukio hilo na kuvishukuru vikosi vya usalama kwa kuilinda.

Nchi ya Haiti imekumbwa na ghasia kwa miezi kadhaa baada ya magenge ya kihalifu kuvamia magereza, kuwaachilia maelfu ya wafungwa na kumlazimisha waziri mkuu kujiuzulu.

"Kufuatia tukio la jana karibu na tovuti yetu kwenye Rue Pavee, vikosi vya usalama na timu ya usalama ya benki hiyo ilifanya kazi kwa weledi na ufanisi. shukrani nyingi kwa maofisa wetu na polisi wa serikali kwa umakini wao". Alisema taarifa ya benki kuu ya nchi hiyo.

Mfanyakazi mmoja alisema watatu au wanne wa genge hilo la wahalifu waliuawa katika shambulio hilo. **BBC**

## Russia yateka mji mwingine Ukraine

**MOSCOW,** RUSSIA

SERIKALI ya Russia imetangaza kuwa imeteka kijiji kingine cha Ukraine, huku ikiwaondoa raia wake 9,000 katika mkoa wa Belgorod kutokana na mashambulizi makali.

Russia imeshuhudia mfululizo wa mashambulizi kutoka vikosi vinavyoiunga mkono Ukraine, vilivyotajwa kama wasaliti na Rais Vladmir Putin.

Wizara ya Ulinzi, ilisema vikosi vyake vimekamata kijiji cha Orlivka, karibu na mji wa viwanda ulioharibiwa wa Avdiivka ambao uliangukia mikononi mwa Warrusia zaidi ya mwezi mmoja uliopita.

Ukraine inapambana dhidi ya uvamizi wa nchi hiyo kwa zaidi ya miaka miwili na ikisaidiwa karibu na mataifa ya Magharibi.

Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Lloyd Austin, ameonya kuwa hatima ya Ukraine iko mashakani wakati ambapo spika wa bunge la wawakilishi Mike Johnson amekataa kuitisha kura nyingine ya kuamua juu ya msaada wa dola bilioni 60 kwa ajili ya taifa hilo. **DW**

# STARS YAKOMAA NA BARIDI WAKIJIFUA KUIVAA BULGARIA

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuwa na hali ya hewa ya baridi kali katika mji wa Baku Azerbaijan, wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wameendelea vyema na programu za mazoezi kwa ajili ya michezo miwili ya kirafiki na kimataifa itakayochezwa nchini humo, imeelezwa.

Kikosi cha Taifa Stars kinaundwa na idadi kubwa ya wachezaji wanaoishi Dar es Salaam, jiji ambalo kwa sasa hali ya hewa ni joto.

Stars ipo katika mji wa Baku kwa ajili ya kuivaa Bulgaria na Mongolia, mechi zitakazochezwa katika tarehe zinazotambulika na Kalenda ya FIFA.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaimu Kocha Mkuu wa Stars, Hemed Suleiman 'Morocco' alisema mara ya kwanza wachezaji wake walionekana kupata wakati mgumu walipofika kwenye uwanja wa mazoezi lakini baada ya dakika 45 nyota hayo walianza kuizoea changamoto hiyo.

Morocco alisema jana kikosi chake kilifanya mazoezi vizuri na anaamini wataonyesha kiwango kizuri katika michezo hiyo miwili ya kirafiki ya kimataifa watakayocheza.

"Ni kama wamekubaliana na hali ilivyo, mara ya kwanza ilionekana kuwaathiri, lakini sasa hivi wanaendelea vyema na programu ya mazoezi, kila kitu kinafanyika kama tulivyotarajia," alisema Morocco.

Kocha huyo alisema kwa sasa kuna mchezaji anaonekana yuko tayari kutimiza majukumu atakayopewa kutokana na kuzoea taratibu hali ya baridi.

"Hatuna jinsi hali ya hewa ni baridi sana, siku ya kwanza tulipofika na ilichukuwa dakika 45 wachezaji kuanza kukubali hali ya hewa hiyo, tunaamini tutakuwa na mchezo mzuri dhidi ya Bulgaria.

Lakini ni mapema sana kueleza hali hii itaathiri kwa kiasi gani programu, haikwepeki, tunatakiwa kuzoea hii baridi kwa sababu haya mazingira ndio tunacheza mechi zetu zote mbili," alisema Morocco.

Stars itacheza mechi yake ya kwanza ya kirafiki dhidi ya Bulgaria kesho na Machi 25, mwaka huu itawavaa Mongolia.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Olimpiki Baku kwa ajili ya kujiandaa kuivaa Bulgaria katika mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa kesho nchini Azerbaijan. **PICHA: TFF**

# Yao kinara 'asisti' mabeki

**Na Adam Fungamwango**

NYOTA wa Yanga, Yao Kouassi, anaongoza kwa kutoa pasi nyingi zilizozaa mabao katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara kwa upande wa walinzi hadi kufikia raundi ya 21.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa jana na Bodi ya Ligi, beki huyo raia wa Ivory Coast, pia anashika nafasi ya pili kwa 'asisti' za jumla, kinara wake ni Kipre Junior wa Azam FC, ambaye ametoa pasi za mwisho nane.

Yao anafuatiwa na beki wa kushoto, Mtanzania anayeichezea KMC FC, Rahim Shomari, ambaye ana 'asisti' tano.

Mabeki Watanzania wawili wa Simba, Shomary Kapombe na Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' wanafuatia kila mmoja akiwa na 'asisti' nne huku Lusajo Mwaikenda, beki mbili wa Azam FC, na mwenzake anayecheza upande wa kushoto katika timu hiyo, Pascal Msindo, wana 'asisti' nne kila mmoja.

Beki wa kushoto wa Yanga, Nickson Kibabage naye ana 'asisti' nne, pamoja na kutopata nafasi ya mara kwa mara katika kikosi hicho cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, lakini kila anapopangwa anaonyesha ubora na kuingia katika rekodi ya mabeki wenye 'asisti' nyingi.

Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha Kalenda na Fifa, huku pia Simba na Yanga zikiwa na majukumu ya michezo ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## Kikapu Zanzibar yalilia wadhamini

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Mpira wa Kikapu Zanzibar (BFZ), linaendelea na mchakato wa kutafuta makampuni yatakayosaidia kudhamini Ligi Kuu ya mchezo huo ambayo inatarajia kufanyika kuanzia Aprili mwishoni, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Habari wa BFZ, Hussein Karama, alisema mpaka sasa wameshakutana na makampuni mbalimbali kwa ajili ya kufanya mazungumzo na anaamini huenda wakapata majibu chanya.

Karama alisema lengo kuu la kutafuta wadhamini ni kuongeza hamasa na ushindani kwa timu zitakazoshiriki ligi hiyo kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

"BFZ imekuwa ikifanya mazungumzo na makampuni pamoja na taasisi mbalimbali ili kuomba udhamini, tunatarajia endapo tutapata wadhamini, basi ligi yetu itakuwa na ushindani mkubwa kama ilivyokuwa miaka mitano iliyopita," alisema Karama.

Ofisa huyo alisema tangu kuchezwa kwa mashindano ya Kombe la Mapinduzi, timu zote zimehamasika na zinajiandaa kupambana kuwania ubingwa wa kikapu wa Zanzibar.

Aliongeza wanafurahi kuona hamasa na kiu ya wachezaji wa kikapu visiwani humo kurejea na anaamini hali hiyo itaongeza hamasa ya kuibua vipaji vipya.

" Basketball inarejea baada ya kutochezwa mashindano yoyote ya kwa muda wa miaka miwili, hata hivyo bado tunaendelea na kutafuta wadhamini hasa wa Ligi Kuu ili kuleta hamasa, viongozi tunajipanga kuhakikisha ligi itakayochezwa inakuwa nzuri na yenye ushindani kwa sababu kutakuwa na kitu (zawadi), ambayo inagombaniwa," Karama alisema.

Aliongeza endapo BFZ itafanikiwa kupata wadhamini mwezi huu, mwaka huu hakutakuwa na ligi mbili ambazo huchezwa katika Kanda ya Unguja na Pemba na badala yake itafanyika ligi moja ya Zanzibar.

Aliongeza udhamini utakaopatikana utasaidia timu kupata fedha za maandalizi na vifaa.

Alisema ligi ya msimu huu itahusisha timu 20 kutoka Unguja (wanaume timu 16 na wanawake timu nane), huku upande wa Pemba utawakilishwa na klabu 11 za wanaume zikiwa nane zilizobakia ni za wanawake.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SOUTHGATE ATAJWA UNITED
MMILIKI mwenza wa Manchester United, Sir Jim Ratcliffe amemfanya Kocha wa England, Gareth Southgate kuwa chaguo lake kuu kuchukua nafasi ya Erik ten Hag msimu wa joto, na angependa kupata uamuzi kutoka kwa kocha huyo mwenye umri wa miaka 53 mapema. ***(Star)***

### GREALISH KUONDOKA CITY
MANCHESTER City huenda ikamruhusu winga wa England, Jack Grealish mwenye umri wa miaka 28 kuondoka msimu huu wa joto huku wakitafuta fedha za kuboresha kikosi chao. ***(HITC)***

### ISAK AWANIWA NEWCASTLE
MSHAMBULIAJI wa Newcastle United na Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 24, yuko kwenye orodha ya wanaowaniwa na Arsenal huku washikabunduki hao wakilenga kuleta mshambuliaji wakati wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### ARSENAL YAMTAKA GYOKERES
ARSENAL pia inavutiwa na mshambuliaji wa Sporting Lisbon na Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 25. ***(Teamtalk)***

### TONEY AGOMBEWA ENGLAND
KLABU za Tottenham Hotspur, Chelsea na West Ham zote zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 28. ***(Sun)***

### WERNER AITEGA SPURS
MSHAMBULIAJI wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 28 anataka Tottenham Hotspur kuamsha chaguo la kumsajili kabisa msimu huu wa joto kwa euro milioni 17 kutoka kwa klabu mama ya RB Leipzig. ***(Florian Plettenberg)***

### ERIKSEN AMPASHA TEN HAG
KIUNGO wa kati wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 32, amemwambia Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag, hajafurahishwa na kukosa muda wa kucheza. ***(Tipsbladet)***

### MCLACHLAN ATAJWA NEWCASTLE
ALIYEKUWA mkuu wa uajiri wa Chelsea, Scott McLachlan analengwa na Newcastle United kuchukua nafasi ya Mkurugenzi wa Michezo, Dan Ashworth, ambaye anaelekea Manchester United. ***(Team Talks)***

### BUTLAND ATAKIWA RANGERS
KLABU ya Rangers iko tayari kutoa pauni milioni 15 kumnunua mlinda mlango wa England, Jack Butland mwenye umri wa miaka 31, huku nia ya kutaka kucheza Ligi Kuu ya England ikiongezeka. ***(Football Insider)***

### DEMBELE SOKONI EPL
KLABU za Everton, Nottingham Forest na West Ham zinamfuatilia winga, Karamoko Dembele mwenye umri wa miaka 21, ambaye amefanya vyema msimu huu baada ya kujiunga na Blackpool kwa mkopo kutoka klabu ya Ufaransa ya Brest. ***(HITC)***

### NOTTINGHAM MAMBO MAGUMU
RUFAA ya Nottingham Forest dhidi ya kukatwa kwao pointi nne kwa kukiuka sheria za kifedha inaweza kuhatarisha adhabu kuongezwa. ***(Times)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND AIVURUGA MANCHESTER CITY

●●●Mashabiki wamshuhudia akitoka mazoezini akiwa anachechemea ikiwa ni...

**OLSO, Norway**

ERLING Haaland alitoka kwenye mazoezi ya timu yake ya taifa juzi Jumanne akiwa anachechemea akiwaacha mashabiki wa klabu yake, Manchester City wakiwa na wasiwasi kuelekea katika mchezo wao mkubwa dhidi ya Arsenal baada ya mapumziko ya kimataifa.

Mshambuliaji huyo, ambaye alikosa mechi 10 mwanzoni mwa msimu huu kutokana na jeraha, amekuwa muhimu kwa matumaini ya City ya kulibeba taji la Ligi Kuu England, akifunga mabao 18 katika mechi 23 kabla ya kwenda mapumziko ya kimataifa mwezi huu.

Wakati wa Haaland na timu ya taifa ulianza vibaya zaidi kwani alionekana akichechemea nje ya mazoezi Jumanne baada ya kuanguka chini.

Kuonekana kwa Haaland katika maumivu kutakuwa wasiwasi mkubwa kwa City, ambao wana mchezo mkubwa dhidi ya Arsenal unaotarajiwa kuchezwa Machi 31.

Kwa bahati nzuri kwa mashabiki wa Man City, daktari wa timu ya Norway, Ola Sand alijitahidi kupunguza wasiwasi wowote kuhusu hofu hiyo ya Haaland.

„Hakuna shida," alisema Sand akiiambia TV2.

Baada ya ushindi wa City wa robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Newcastle United, Kocha Pep Guardiola aliwataka wachezaji wake kujilinda kwenye majukumu ya kimataifa kabla ya mchezo mkubwa dhidi ya Arsenal.

„Haaland si mchezaji wangu tena kuanzia sasa, kile wachezaji wote watakachoamua kitakuwa sawa," alisema.

„Wanajua kuwa walipigana sana, wanatakiwa kuwa makini kufika katika nafasi hii.

„Wanajua ni michezo ya kirafiki na wanapaswa kucheza kwa busara. Natumaini wanaweza kufanya hivyo," alisema Guardiola.

# FERNANDES AKIRI KUSHUKA KIWANGO

**LISBON, Ureno**

NAHODHA wa Manchester United, Bruno Fernandes amesema anafahamu vyema hayupo kwenye kiwango cha juu huku akielewa matatizo ambayo timu hiyo inakabiliwa nayo msimu huu.

United imejitahidi kuipata kasi yake hadi sasa lakini imejikuta ikipoteza mara 11 tayari kwenye Ligi Kuu na kushuka hadi nafasi ya sita, huku pia ikitolewa katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Fernandes naye hajawa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi msimu huu, lakini amesema anatambua matatizo ya Man United.

"Katika Manchester United haujawa msimu wa mafanikio kibinafsi," alisema katika mkutano na waandishi wa habari.

"Ninafahamu kabisa kwamba nina uwezo wa kufanya zaidi na bora siku zote. Sina wasiwasi na hilo kwa sasa, kwa sababu ninachosema kila mara ni kwamba kujitolea kwangu huwa katika kiwango cha juu, bila kujali ninaiwakilisha Ureno au Manchester United.

"Ndio maana nimetulia kuhusu hilo na ninajua kuwa ubora wa kiwango changu unaweza kuboreka kila wakati."




Msimu huu, Fernandes amecheza mechi 38 katika michuano yote akiwa na United, akifunga mabao nane na kutoa pasi tisa za mabao kwa wakati huo.

Alilazimika kucheza kama beki wa kati wa dharura katika ushindi wa 4-3 wa United dhidi ya Liverpool kwenye Kombe la FA Jumapili, akirudi nyuma pamoja na Harry Maguire katika muda wa ziada.

Kwa sasa, umakini wake unaangazia majukumu ya kimataifa na Ureno, ambapo anatazamiwa kushiriki katika mechi za kirafiki dhidi ya Sweden na Slovenia.

Fernandes na United watarejea kwenye mechi za Ligi Kuu Machi 30 kwa safari ya kwenda London Magharibi kucheza na Brentford.

## Southgate amwita Mainoo England

**LONDON, England**

KIUNGO wa Kati wa Manchester United, Kobbie Mainoo, ameongezwa kwenye kikosi cha wakubwa cha England cha Kocha Gareth Southgate kabla ya mechi ya kimataifa za mwezi huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 amekuwa katika kiwango bora kwa klabu msimu huu, lakini aliachwa nje ya kikosi cha awali cha wachezaji 25 cha Southgate, huku kocha huyo akisisitiza kuwa hataki kumpa shinikizo kubwa Mainoo katika kipindi hiki cha maisha yake ya soka.

Hapo awali Mainoo aliitwa katika kikosi cha vijana chini ya umri wa miaka 21 kwa mara ya kwanza katika maisha yake ya soka, lakini England sasa imethibitisha kwamba atajiunga na kikosi cha wakubwa badala yake.

England imethibitisha kuwa kundi la awali la wachezaji 25 wote waliripoti pale St George's Park siku ya Jumanne, huku Mainoo akijiunga na kundi hilo kwa mechi zijazo za kirafiki.

Mainoo ameiwakilisha England kutoka timu za vijana wa chini ya miaka 17 hadi 19 lakini sasa yuko tayari kukipiga katika kikosi cha wakubwa.

Kupandishwa katika kikosi cha wakubwa cha England kunashuhudia msimu wa kufurahisha wa Mainoo ukiendelea.

Baada ya mechi ya kujiandaa na msimu mpya, kiungo huyo kijana alijikuta akikaa nje ya uwanja kwa zaidi ya miezi miwili kutokana na jeraha la kifundo cha mguu, lakini alionesha ubora mara moja aliporejea uwanjani na kikosi cha United.

Kocha Erik ten Hag amempa Mainoo mechi 20 katika mashindano yote hadi sasa msimu huu, ikiwa ni pamoja na mechi 14 alizoanza kwenye Ligi Kuu England.

Wito wa mechi ya kwanza ya England ulikabiliwa na upinzani kutoka kwa Southgate ambaye, ingawa alithamini kipaji cha Mainoo, aliomba tahadhari na kulinganisha hali hiyo na kuibuka kwa Bukayo Saka na Jude Bellingham, ambao wote walikuwa na uzoefu wa juu mara mbili kabla ya kuanza kwa mara ya kwanza kuichezea timu ya taifa.

Hata hivyo, Mainoo sasa ana nafasi ya kuchezea kikosi chake cha kwanza katika mechi zijazo za kirafiki dhidi ya Brazil na Ubelgiji zitakazofanyika kwenye Uwanja wa Wembley.



## Courtois majanga tena aumia goti

**MADRID, Hispania**

GOLIKIPA wa Real Madrid, Thibaut Courtois amepata jeraha jipya la goti ambalo lilimlazimu kuondoka kwenye mazoezi ya Jumanne huku akilia.

Courtois hajaichezea Madrid msimu huu baada ya kuumia nyama za paja wakati wa majira ya joto, lakini alikuwa akifanya mazoezi na timu hiyo siku chache zilizopita na alitarajiwa kurejea uwanjani baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa Machi.

Hata hivyo, nafasi yake ya kucheza kabisa msimu huu imepata pigo kubwa baada ya kupata jeraha jipya la goti wakati wa mazoezi.

"Baada ya vipimo vilivyofanywa jana kwa mchezaji wetu Thibaut Courtois, amegundulika kuwa amechanika nyama ndani ya goti lake la kulia," ilisema taarifa ya klabu hiyo. Jeraha lilitokea wakati wa mazoezi."

Muhimu zaidi, jeraha sio kwa goti lile lile ambalo Courtois aliumia wakati wa msimu wa joto uliopita.

Ripoti zinasema kuwa Courtois alipelekwa mara moja kwa uchunguzi ambao ulibaini anatarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa angalau wiki sita.

Kutokuwapo kwa wiki sita kutamfanya Courtois awe huru kurejea mapema Mei, ikiwa ni mwezi wa mwisho kwa LaLiga msimu huu ambapo ligi hiyo itafikia tamati Mei 26, hata hivyo muda huo wa kukaa nje unaweza kuongezwa ikiwa kipa huyo atahitaji upasuaji.

Katika nafasi ya Courtois, Andriy Lunin ameng'ara msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ukraine anatarajiwa kupewa mkataba mpya, baada ya kupambana na mchezaji aliyecheza kwa mkopo Kepa Arrizabalaga katika chaguo la kwanza msimu huu.

Kepa alisajiliwa kutoka Chelsea msimu uliopita wa joto baada ya Courtois kuumia awali na mara moja akachukua nafasi ya Mbelgiji huyo kwenye timu, kwa sababu ya jeraha dogo tu lililofungua mlango kwa Lunin ambaye kiwango chake cha kuvutia kimemaliza mapendekezo ya Madrid kumsajili Kepa kabisa msimu huu wa joto.



HABARI MICHEZO

# NDUMBARO ASISITIZA UWEKEZAJI AKIZINDUA MTANDAO WA SIMBA

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, amezitaka klabu ambazo zinamilikiwa na wanachama kujenga mifumo mizuri ya uwekezaji ili kujiendesha zenyewe badala ya kutegemea wafadhili fedha kutoka kwa watu binafsi, imeelezwa jijini Dar es Salaam juzi usiku.

Ndumbaro alisema hayo wakati wa uzinduzi wa Simba Executive Networks wenye lengo la kukusanya fedha ili kuendeleza miundombinu ya klabu ya Wekundu wa Msimbazi ikiwamo Uwanja wa Mo Simba Arena.

Simba Executive Networks itaongozwa na Mwenyekiti wake, Abdul-Razaq Badru huku mlezi akiwa Naibu Spika, Mussa Azan Zungu.

Ndumbaro alisema viongozi wanatakiwa kuweka mfumo mzuri utakaowezesha wanachama kuchangia klabu yao katika mambo muhimu ikiwamo kujiimarisha kiuchumi katika klabu hizo.

Alisema Tanzania imepiga hatua katika mchezo wa soka na Ligi Kuu Bara inashika nafasi ya sita huku Simba ikishika nafasi ya saba barani Afrika, hadhi ya ligi iendane na hadhi ya klabu hasa ubora wa miundo mbinu pamoja na kuanza kujitegemea.

"Kuongoza timu sio lele mama, Mo Dewji (Mohammed Dewji), anatakiwa kupongezwa, lakini tukumbuke huyo ni mwanadamu, viongozi tukishirikiana na mpango huu wa Simba Executive Networks tunatengeneza wawekezaji wengine na kuifanya Simba iwe bora katika vitega uchumi maradufu.

Ni vizuri kuangalia mfumo mpya ambao utashirikisha watu kila pembe ya dunia ili kupata wanachama wapya na kutoka kwenye ushabiki kuwa wanachama kamili. Soka la Tanzania linazidi kukua, mafanikio ya klabu zetu kimataifa ni dhahiri sasa Simba imefanya vizuri takribani miaka 10 sasa huku Yanga miaka miwili," alisema Ndumbaro na aliongeza;

Sasa ni muda wa kutafakari mafanikio hayo tunayapataje lakini muda huu kuuangalia jinsi gani ya timu zote mbili zinakwenda nusu fainali, wikiendi hii Watanzania wote tunaungana kusapoti timu zetu kwa kujitokeza uwanjani na kuacha itakadi zetu za Usimba na Yanga.

Alieleza serikali haifurahishwi na baadhi ya Watanzania kuwafanya wageni kuona wako nyumbani na kuagiza tabia hiyo inatakiwa kumalizika huku akionya timu itakayokiuka itachukuliwa hatua.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema mtandao huo utaongozwa na viongozi waandamizi ambao moja ya kazi zao ni kuhakikisha miradi ya klabu inasimamiwa na kufanyiwa kazi.

"Ili kuwa mwanachama wa mtandao huu unatakiwa kulipia kiasi cha Sh. milioni 1.5 kwa mwaka na utaruhusiwa kulipa kwa miezi mitatu, sita au kwa mkupuo.

Kajula alitaja baadhi ya vitu anavyopata mwanachama wa Simba Executive Networks ni jezi mpya za kila msimu, tiketi za mechi kubwa na za kimataifa, Bima ya maisha, kutumia miradi yetu kama Uwanja wetu wa Simba Mo Arena kucheza mechi za mabonanza na kufurahia," alisema Kajula.




Wasanii wakicheza ngoma za asili za kabila la Wasukuma wakati wa uzinduzi wa Tamasha la Kimataifa la Utamaduni na Utalii maarufu Lake Zone Cultural and Tourism Festival uliofanyika kwenye Uwanja wa CCM Bariadi mkoani, Simiyu hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kanuni zaja kuibeba Al Hilal

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB), imesema baada ya Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Soka Nchini (TFF), kubariki Al Hilal ya Sudan kushiriki katika Ligi Kuu msimu ujao, mchakato umeanza kwa kubadilisha kanuni.

Ofisa Mtendaji wa Bodi hiyo, Almasi Kasongo, alisema jana kwa sasa ni kazi ya Sekretarieti ya TFF na Bodi ya Ligi kutengeneza kanuni zitakazoiruhusu timu hiyo kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Kama Kamati ya Utendaji TFF imebariki, imeazimia, sasa ni kazi ya Sekretarieti ya Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), na Sekretarieti ya Bodi ya Ligi, kutengeneza kanuni ambayo itakuwa inatoa ruksa ya Al Hilal ya Sudan kuwa sehemu ya ligi yetu, itakuwaje? Kwa sababu ni timu ya Sudan lakini wanashiriki ligi ya Tanzania, kwa mazingira gani? Kwa utaratibu gani? Kanuni ndizo zitakuwa mwongozo wa yote," alisema Kasongo.

Alisema baada ya kutengenezwa kanuni zitatolewa kwa wadau wote wa michezo ambao watatoa maoni yao kabla ya kuchakatwa na kuwekwa rasmi kwa ajili ya utekelezwaji.

"Tutaweka mazingira vizuri, mfano ikitokea wao wakawa nafasi ya kwanza, ya pili, ya tatu, itakuwaje? Itakuwa ikipata pointi itakapokuwa inashinda mechi zake, au isiwe inapata?" Kasongo aliongeza.

Timu za Sudan zimekuwa zikipiga hodi katika nchi mbalimbali kuomba kucheza ligi kwa ajili ya kuwapa utimamu wa mwili wachezaji wake kabla ya mechi za kimataifa kutokana na kutoshiriki ligi ya nyumbani kwao kwa sababu ya vita za wenyewe kwa wenyewe.

## Simba: Tunaitaka nusu fainali Afrika

INATOKA UK. 24

Uongozi wa Simba umesema mikakati ya benchi la ufundi la timu hiyo ambalo liko chini ya Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, limepanga kumaliza hatua ya robo fainali nyumbani kwa kupata mabao mengi ili kujiweka kwenye mazingira mazuri.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili uongozi wa timu hiyo umepanga kumpa kila anachohitaji Benchikha ili kuhakikisha Wamisri 'wanakufa' hapa Dar es Salaam.

„Hii ni mechi muhimu sana Wanasimba, Kocha Benchikha anaendelea kukisuka kikosi kuwa imara, kikosi kimeenda visiwani Zanzibar kwa siku nane kwa ajili ya maandalizi na wakiwa visiwani humo watapata muda mzuri wa kukamilisha programu yake ya mazoezi ambayo ni mara mbili kwa siku," alisema Ahmed.

Aliongeza wakiwa Zanzibar watapata nafasi ya kufanya mazoezi usiku, muda sawa wa mechi yao na kusema hawana wasiwasi wowote.

"Kwa ukubwa tuliokuwa nao Simba hatuna wasiwasi na muda wowote ambao tutapangiwa kucheza, kikosi chetu kipo tayari kucheza muda huu na tumedhamiria kumfanya vibaya Al Ahly," Ahmed aliongeza.

Alimtaja mwamuzi wa kati wa mchezo huo ni Abongile Tom atakayesaidiwa na Zakhele Thusi (Afrika Kusini), Dimbiniaina Andria Tianarivelo (Madagascar) na Jelly Afred wa Afrika Kusini.

„Katika mchezo huo tunaenda na kauli mbiu yetu ya 'Tunaitaka Nusu Fainali', robo fainali nne zilizopita zimetuimarisha na sasa tunaenda kupambana na Al Ahly kutafuta tiketi ya kwenda kucheza nusu fainali," alisema Ahmed.

Aliongeza licha ya kutaka kutinga hatua nusu fainali, lakini wanafahamu hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu wanaenda kucheza na mpinzani mgumu na mwenye ubora.

## Hatima ya Pacome, Kouassi kitendawili

INATOKA UK. 24

wapya wanaoweza kuziba pengo hilo endapo itabainika Yao na Pacome, hawatakuwa sehemu ya mchezo huo.

„Kocha ameanza kutengeneza mikakati ya kuangalia hata kama hawakuwapo nini kifanyike, nani atachukua nafasi yao, kwa hiyo ameanza kuandaa mbinu mbadala, ili ikitokea kama hawatakuwapo, wachezaji watakaocheza wawe tayari kwa mapambano," kilisema chanzo chetu.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, ambaye awali alisema baada ya saa 72 tangu kumalizika mchezo wao dhidi ya Azam, wanachama na mashabiki wa Yanga watafahamu hali za wachezaji wao, jana hakupatikana kuzungumzia sintofahamu hiyo.

Yanga ambayo msimu uliopita ilicheza fainali za mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, ndio vinara na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Michezo

Alhamisi Machi 21, 2024

Nipashe

**Haaland aivuruga Manchester City**

UKURASA 21





Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly itakayochezwa Machi 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

# SIMBA: TUNAITAKA NUSU FAINALI CAF

## ●●●Rais Samia aongeza dau, kununua bao Sh. mil. 10, kilio cha uzalendo...

**Shufaa Lyimo na Saada Akida**

WAKATI Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amesema atanunua kila bao litakalofungwa katika mechi za robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Sh. milioni 10, Simba imetamba inataka kumaliza hatua hiyo katika dakika 90 za nyumbani.

Simba itacheza mechi ya robo fainali dhidi ya Al Ahly kutoka Misri Machi 29, mwaka huu wakati siku inayofuata Yanga itarusha karata yake dhidi ya Mamelodi Sundowns kutoka Afrika Kusini, mechi zote zitachezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, baada ya kumaliza kikao na viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Bodi ya Ligi Kuu (TPLB), Simba na Yanga, Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, alisema Rais Samia ameongeza dau hilo ili kuwaongezea hamasa wachezaji.

„Mama Samia ameongeza dau, sasa atatoa Sh. milioni 10 kwa kila goli badala ya milioni tano alizokuwa anazitoa katika michezo iliyopita kwa sababu anataka timu zote ziingie hatua ya nusu fainali,“ alisema Ndumbaro.

Waziri huyo pia amewataka viongozi wa Simba na Yanga washirikiane na serikali kwa lengo la kupanga mikakati ya kuhakikisha wanasonga mbele katika mashindano hayo.

Alisema huu ni wakati wa Watanzania kuonyesha uzalendo kwa kujitokeza kwa wingi uwanjani kuzishangilia timu hizo ili kuweka historia mpya.

Aliongeza kwa upande wa serikali maandalizi yanaendelea vizuri na kusema wameandaa usalama wa kutosha kuanzia eneo la uwanja na watahakikisha kila Mtanzania anapata tiketi ya kuingia uwanjani kirahisi.

Waziri huyo aliwataka wasemaji wa klabu hizo waache tabia ya kubezana na badala yake waangalie maneno ya kuzungumza kuelekea katika michezo hiyo ya kimataifa.

Naye Rais wa (TFF), Wallace Karia, alisema timu hizo zikifanikiwa kusonga mbele, idadi ya timu zitakazoshiriki michuano hiyo ya kimataifa zitaongezeka.

Karia alisema yoyote atakayekwenda kinyume na taratibu zilizoweka atachukuliwa hatua na kuongeza anataka kuona Tanzania inafika mbali katika michezo.

Imani Kajula, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba alisema wamejipanga vyema kupata matokeo chanya katika mchezo huo na wanamshukuru Mama Samia kutokana na hamasa anazoendelea kuzitoa.

„Lengo letu ni kuingia hatua ya nusu fainali, tunaomba Watanzania waje kwa wingi wajaze uwanja ili tuvuke hatua ya robo fainali, „ alisema Kajula.

Mtendaji Mkuu wa Yanga, Andre Ntime, alisema malengo yao ni kufanya vizuri huku akiomba Watanzania wadumishe uzalendo.

INAENDELEA UK. 23



## Hatima ya Pacome, Kouassi kitendawili

**Na Adam Fungamwango**

HUKU taarifa rasmi kuhusiana na afya ya nyota wawili tegemeo wa Yanga, Yao Kouassi na Pacome Zouzoua, ikiwa haijatolewa, Kocha Mkuu wa vigogo hao, Miguel Gamondi, amesema ameanza kuandaa wachezaji wakaoziba pengo endapo atawaokoa katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundowns kutoka Afrika Kusini, imeelezwa.

Yanga itawaalika Mamelodi Sundowns katika mechi ya robo fainali ya michuano hiyo ya kimataifa itakayochezwa kuanzia saa 3:00 usiku Machi 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mpaka jana jioni hakuna taarifa rasmi kuhusiana na maendeleo ya wachezaji hao ambao waliumia katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC iliyochezwa mapema wiki hii.

Pacome aliumia goti na Kouassi alipata tatizo la misuli ya nyama za paja kwenye mechi hiyo iliyomalizika kwa Yanga kufungwa mabao 2-1.

Meneja wa Yanga, Walter Harrison, alisema anaamini wachezaji hao watapona mapema kabla ya mechi hiyo muhimu.

„Mashabiki wetu wasiwe na wasiwasi, madaktari wetu wanafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha nyota hao wanarejea kwenye hali ya kawaida, ingawa bado madaktari hawajatoa taarifa rasmi, lakini naamini majeraha yao hayataweza kusababisha wasicheze mechi hiyo kwa sababu muda wa kupona bado upo,“ alisema Harrison.

Mbali na wachezaji hao, Yanga inakabiliwa na majeruhi wengine kama Khalid Aucho aliyefanyiwa upasuaji hivi karibuni na Zawadi Mauya.

Taarifa kutoka Yanga zinasema Gamondi ameanza kukiangalia upya kikosi chake na kwa kupanga nyota

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >